View metadata, citation and similar papers at core.ac.uk brought to you by CORE
provided by Digital Library of Open University of Tanzania

# MTINDO KATIKA RIWAYA YA MARIMBA YA MAJALIWA YA EDWIN SEMZABA

**MARTHA ISAACK SILAVWE**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2016**

## UTHIBITISHI

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo ***Mtindo katika Riwaya ya Marimba ya Majaliwa ya Edwin Semzaba,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya Mashart ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi, **Martha Isaack Silavwe**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

………………………………

Saini

………………………………

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku Tasinifu hii kwa Mume wangu mpenzi Joshua Josephat Nyivambe Sanga na watoto wetu wapenzi Glory Joshua na Godlove Joshua. Pia naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu akiwemo baba Isaack Silavwe na mama Sara Nakamanga.

## SHUKURANI

Shukurani za dhati nazitoa kwa Mwenyezi Mungu baba muweza wa yote kwa kunipa uzima ulionifanya nifike katika kukamilisha tasinifu yangu. Kama si kuwa na afya nzuri katika kipindi chote cha masomo nisingeweza kufanikisha kazi hii.

Pia, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Dr. Mohamed Omary Maguo kwa kuniongoza katika kuandaa pendekezo la utafiti mpaka hii leo nimefikia hatua ya kuwasilisha tasinifu yangu. Natambua kuwa kuna wakati aliacha kazi zake na hata usingizi ili aweze kuisoma kazi yangu na kuifanyia marekebisho ya msingi. Sina neno kwake la kumfanya aelewe nimemshukuru zaidi ya kusema, “Asante sana na Mungu akubariki”.

Kipekee napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa walimu wangu wapendwa walionifundisha kozi mbalimbali darasani. Walimu hao ni Prof. Tigiti Sengo, Prof. Emmanuel Mbogo, Dr. Anna Kishe, Dr. Hadija Jilala, Dr. Mohamed Omary na mwalimu Nasra Habibu. Nawashukuru sana walimu wangu kwa mafunzo mliyonipatia hata leo nimeweza kukamilisha tasinifu yangu.

Mwisho napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu kwa kunivulia katika kipindi chote cha masomo ambapo nilikuwa mbali nao. Namshukuru sana mume wangu bwana Joshua Josephati Sanga kwa uvumilivu wake pamoja na watoto wetu Glory Joshua na Godlove Joshua.

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchambua matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Malengo mahususi yalikuwa mawili ambayo ni kuchambua matumizi ya mtindo yanayohusiana na lugha katika riwaya ya Marimba ya Majaliwa na kubainisha matumizi ya mtindo yanayohusiana na vipengele vinginevyo vya kimtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Data hizo zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Simiotiki. Kwa upande wa lengo mahususi la kwanza, matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa matumizi ya kimtindo ya lugha ni pamoja na tamathali za usemi za tashibiha, chuku na takriri. Pia kuna matumizi ya methali na Kiswahili cha kimaeneo. Kwa upande wa lengo mahususi la pili, matokeo ya utafiti ni kuwa vipengele vingine vya kimtindo vilivyotumika katika riwaya teule ni matumizi ya nyimbo, hadithi ndani ya hadithi, mwingiliano matini, tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu na uhalisia mazingaombwe.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHI** ........ ii

**HAKIMILIKI** ........ iii

**TAMKO** ........ iv

**TABARUKU** ........ v

**SHUKURANI** ........ vi

**IKISIRI** ........ vii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI** ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........ 5

1.4 Malengo ya Utafiti ........ 6

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ........ 6

1.4.2 Malengo Mahususi ........ 6

1.4.3 Maswali ya Utafiti ........ 6

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 7

1.6 Mipaka ya Utafiti ........ 7

1.7 Mpangilio wa Tasinifu ........ 8

**SURA YA PILI** ........ 9

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ........ 9

2.1 Utangulizi ........ 9

2.2 Dhana ya Mtindo ........ 9

2.3 Fasihi ya Watoto ........ 10
2.4 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti ........ 11
2.5 Mapitio kuhusu Marimba ya Majaliwa ........ 17
2.6 Mkabala wa Kinadharia ........ 18
2.6.1 Nadharia ya Simiotiki ........ 19
2.7 Pengo la Maarifa ........ 23
2.8 Hitimisho ........ 23
**SURA YA TATU** ........ 24
**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ........ 24
3.1 Utangulizi ........ 24
3.2 Eneo la Utafiti ........ 24
3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 25
3.4 Aina ya Utafiti ........ 25
3.5 Kundi Lengwa ........ 26
3.6 Sampuli na Usampulishaji ........ 26
3.7 Aina ya Data Zilizokusanywa ........ 27
3.7.1 Data za Msingi ........ 27
3.7.2 Data za Upili ........ 28
3.8 Ukusanyaji wa Data ........ 28
3.8.1 Usomaji Makini ........ 28
3.8.2 Upitiaji wa Nyaraka ........ 29
3.9 Mbinu za Uchambuzi wa Data ........ 30
3.9.1 Mkabala wa Kimaelezo ........ 30
3.10 Usahihi wa Data za Utafiti ........ 30

3.11 Maadili ya Utafiti ........................................................................................ 31

3.12 Hitimisho......................................................................................................... 31

**SURA YA NNE**......................................................................................................... 32

**4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI** ............................................................................................................. 32

4.1 Utangulizi ........................................................................................................ 32

4.2 Matumizi ya Vipengele vya Lugha vya Kimtindo ........................................ 32

4.2.1 Matumizi ya Tashibiha ................................................................................. 33

4.2.2 Matumizi ya Chuku ...................................................................................... 35

4.2.3 Matumizi ya Takriri ...................................................................................... 38

4.2.4 Matumizi ya Methali ..................................................................................... 40

4.2.5 Matumizi ya Kiswahili cha Kimaeneo .......................................................... 42

4.3 Vipengele Vingine vya Kimtindo katika Marimba ya Majaliwa ................... 43

4.3.1 Matumizi ya Nyimbo .................................................................................... 44

4.3.2 Matumizi ya Hadithi Ndani ya Hadithi ......................................................... 46

4.3.3 Mwingiliano Matini katika Riwaya ya Marimba ya Majaliwa ...................... 47

4.3.4 Mtindo wa Tanzu Ndani ya Tanzu Ndani ya Tanzu ...................................... 49

4.3.5 Mtindo wa Uhalisia Mazingaombwe ............................................................. 50

4.4 Hitimisho......................................................................................................... 52

**SURA YA TANO** ...................................................................................................... 53

**5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............................ 53

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 53

5.2 Muhtasari......................................................................................................... 53

5.2.1 Vipengele vya Kimtindo vya Matumizi ya Lugha ........................................ 53

5.2.2 Vipengele vingine vya Kimtindo katika Riwaya Teule ................................. 54

5.3 Mapendekezo ....................................................................................... 55

**MAREJELEO** ........................................................................................... 56

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu kuchunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* iliyoandikwa na mtunzi maarufu Edwin Semzaba. Mwandishi huyu ni maarufu kutokana na utunzi wa tamthiliya ya *Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe* ambayo inatumika katika shule za sekondari kama kitabu cha kujisomea. *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya mpya iliyoandikwa mahususi kwa ajili ya watoto na hivyo bado haijafanyiwa utafiti wa kutosha katika maeneo mbalimbali likiwepo hili la mtindo. Kutokana na hali hii tukaona ipo haja ya msingi ya kufanya utafiti huu ili kuweza kutoa mchango wetu katika kuziba pengo hili la maarifa. Katika sura hii ya kwanza tumeshughulikia vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Utunzi wa kazi za fasihi iwe simulizi au andishi huegemea katika maudhui na fani ambapo mambo haya mawili hutegemeana na kukamilishana (Madumullah, 2009). Hakuna kazi ya fasihi ambayo inaweza kuandikwa bila ya kuwa na mambo haya mawili halafu bado kazi hiyo ikaendelea kuitwa kuwa ni kazi ya fasihi. Maudhui katika kazi ya fasihi hujumuisha vipengele vya dhamira, ujumbe, falsafa, migogoro, msimamo na mtazamo wa mwandishi (Khamis, 2007). Fani kwa upande wake hujumisha muundo, mtindo, wahusika, matumizi ya lugha na mandhari (Msokile,

1992; 1993). Katika utafiti huu tumechukuwa kipengele cha mtindo kama jambo la kushughulikiwa kiutafiti katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kwa lengo la kufanikisha azma ya utafiti huu.

Mtindo ni kipengele cha fani ambacho huelezwa na wataalamu wa fasihi kama ni namna au jinsi mtunzi wa kazi ya fasihi anavyoisana kazi yake na kuiwasilisha kwa hadhira iliyokusudiwa kwa ujembe na dhamira ile ile aliyotaka hadhira iipate (Wamitila, 2008). Matumizi ya mtindo katika kazi za fasihi ndicho kipengele ambacho kinatajwa kuwa humtofautisha mtunzi mmoja na mwingine. Hii inatokana na ukweli kwamba kila mtunzi anao mtindo wake wa kuwasilisha jambo mbele ya hadhira yake kwa namna ambayo yeye binafsi anaona kuwa ni sahihi kufanya hivyo. Kwa mfano, matumizi ya mtindo katika riwaya za Shaaban Robert ni tofauti sana wa mtunzi Euphrase Kezilahabi katika utunzi wake wa riwaya. Uteuzi wa mtindo katika kazi za riwaya na fasihi kwa jumla hutegemea ubunifu, uzoefu na ugunduzi wa mwandishi katika utunzi wa riwaya.

Matumizi ya mtindo ni kipengele cha kifani ambacho ni mardudi katika kazi za fasihi si tu katika fasihi ya Kiswahili bali katika fasihi zote duniani (Mlacha, 1989; 1991). Kipengele hiki hujitokeza kwa namna za aina kwa aina kama vile matumizi ya lugha, mwingiliano matini, mwingilianao wa tanzu, matumizi ya barua, namna ya kuelezea visa na matukio, matumizi ya vina na mizani katika mashairi, mtindo wa mashairi huru, uteuzi wa aina za wahusika na uteuzi wa visa na matukio (Hawthorn, 1985). Hata hivyo, katika ulimwengu wa fasihi ya Kiswahili, kipengele cha mtindo hufafanuliwa na wataalamu kwa maneno na mifano michache tu ambayo haifafanuwi

kwa undani juu ya kipengele hiki ambacho ndicho kinachotumika kuwavutia wasomaji na wasikilizaji wa kazi za fasihi. Hali hii imetusukuma kufanya utafiti huu ili hatimaye tuweze kutoa mchango wetu katika kupanuwa uelewa kuhusu mtindo katika kazi za fasihi kwa kuchambua mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Katika tasinia ya riwaya ya Kiswahili wapo wataalamu kadhaa ambao wametafiti matumizi ya mtindo katika riwaya wakirejelea riwaya za watunzi wa zamani kama vile Shaaban Robert kupitia riwaya zake za *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Adili na Nduguze* na *Siku ya Watenzi Wote* kuzitaja kwa uchache. Mohamed (2006) aliandika makala iliyochunguza matumizi ya mtindo katika riwaya za Shaaban Robert. Katika makala hayo, amebainisha mitindo mbalimbali iliyotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira huku mtindo alioulezea zaidi ni ule wa matumizi ya uwili. Hii ina maana katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* kila jambo hutajwa kutokana na uwili wake kama vile kila unapotajwa msikiti na kanisa pia hutajwa, kila inapotajwa dini ya Kiislamu na ile ya Kikristo pia hutajwa, panapotajwa mbingu na ardhi pia hutajwa, anapotajwa mwanamke na mwanaume pia hutajwa na huendelea hivyo hivyo. Huu ni mtindo wa pekee kwa mtunzi huyu kwani haujaonekana kutumiwa na waandishi wengine wa siku hizi kwa ufanisi kama alivyoutumia Shaaban Robert. Mtindo wa aina hii ni mzuri kwani huwagusa hadhira wa aina zote na hivyo kuwa ni njia rahisi ya kufikisha ujumbe kwao wote. Kazi ya Mohamed (ameshatajwa) imetupatia ufahamu zaidi wa kujua namna mtindo unavyojitokeza katika kazi za fasihi na katika utafiti wetu tumeyatumia maarifa haya.

Senkoro (2006) naye ameshughulikia mtindo katika kazi za fasihi japo kwa muhtasari pale alipoandika makala yake juu ya makutano baina ya fasihi simulizi na

andishi. Anaeleza kuwa fasihi andishi ya Kiswahili imechota kipengele cha mtindo kutoka fasihi simulizi na kukifanya kuwa ni cha kwake. Anatolea mfano suala la mwingiliano wa tanzu ni mtindo mkongwe katika fasihi simulizi ambapo tanzu zaidi ya moja hujitokeza katika aina fulani ya utanzu unaowasilishwa. Mathalani, inaweza kuwa ni utanzu wa hadithi ndio unaotambwa kwa wakati huo lakini ndani yake mnajitokeza maigizo, nyimbo, semi na vichekesho. Leo katika fasihi andishi napo kunajitokeza mwingiliano wa tanzu kama huo wa fasihi simulizi. Mawazo haya ya Senkoro (ameshatajwa) yametusaidia kuelewa zaidi dhana ya mtindo ambapo tumefahamu kuwa mwingiliano wa tanzu ni kipengele cha kimtindo na tumekishughulikia katika utafiti wetu.

Walibora (2010) aliandika makala juu ya uhalisia na uhalisiamazingaombwe akilinganisha riwaya za *Dunia Yao* na *The Tin Drum*. Anabainisha kuwa riwaya ya Kiswahili hususani Dunia Yao na zile za Kezilahabi, Wamitila na Mkufya zimepiga hatua katika matumizi ya mtindo kiasi cha kuendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Maisha ya jamii ya leo yamekuwa magumu yenye visa na masaibu mengi yasiyoelezeka kwa urahisi. Riwaya mpya ya Kiswahili imelazimika kuwa na aina ya mtindo ambao unafungamana na hali hiyo ya maisha ya jamii katika karne ya ishirini na moja. Mtindo wa uteuzi na uelezeaji wa visa na matukio nao ni wa kihalisiamazingaombwe. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Yao*, mtunzi anapendekeza kuwa ili kutatua changamoto ya msongamano wa magari katika jiji la Nairobi ni sharti magari mengine yawe yanapaa juu. Katika maisha halisia ya jamii ya leo si jambo halisi gari kupaa juu bali ni ndege tu zenye uwezo huo. Hata hivyo, halikuwa lengo la mtunzi wa riwaya hiyo kutaka magari yapae juu kwa mkabala huo

usio wa kiuhalisia, anachopendekeza hapo ni kujengwa kwa barabara za juu al-maarufu kwa jina la "Flying Overs" ili kupunguza msongamano wa magari maeneo ya mjini.

Mawazo ya Walibora (ameshatajwa) yametusaidia kufahamu kwamba matumizi ya mbinu za kiuhalisiamazingaombwe katika riwaya ni moja kati ya vipengele vya kimtindo. Utafiti wake ulijikita katika riwaya zinazojulikana kama riwaya za kisasa lakini hata katika Riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ambayo ni riwaya ya watoto mna matumizi ya mtindo wa kiuhalisiamazingaombwe. Mawazo haya tuliyachukua na kuyafanyia kazi katika tasinifu hii.

Wataalamu hao tuliowataja hapo juu pamoja na kazi zao wameshughulikia kipengele cha mtindo kwa namna tofautitofauti kama tulivyobainisha. Kati ya wanazuoni hao hakuna hata mmoja ambaye amechunguza kipengele cha mtindo katika riwaya ya watoto na kubainisha namna mtindo ulivyotumika katika riwaya hiyo. Katika utafiti wetu tuliliona hili kama ni pengo la maarifa ambalo tunatakiwa kulifanyia utafiti ili kukuza maarifa juu ya riwaya ya Kiswahili na hasa kipengele cha mtindo. Pengo hili la maarifa limejazwa kutokana na kuchunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

*Marimba ya Majaliwa* ni riwaya ya watoto iliyopata tunzo ya kwanza ya uandishi bora wa riwaya za watoto. Riwaya hii kwa sifa yake kwamba ni riwaya ya watoto itakuwa na matumizi ya mtindo ambayo kwa kiasi kikubwa yanalandana na dhamira zinazowahusu watoto. Matumizi hayo ya mtindo katika riwaya za watoto bado

hayafahamiki kwa sababu hakuna utafiti uliofanywa katika kuchunguza kipengele hiki. Watafiti watangulizi wamevutiwa na riwaya zilizolengwa kwa ajili ya watu wazima na vijana. Wataalamu hao ni Mohamed (2006), Senkoro (2006) na Walibora (2010). Pengo hili la maarifa limetufanya tufanye utafiti wa kuchunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kwa lengo la kubainisha mitindo mbalimbali inayojitokeza katika riwaya hiyo na hatimaye kuwa tumetoa mchango wetu wa kufahamika kwa mtindo wa riwaya za watoto.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahususi mawili.

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni pamoja na:

i) Kuchambua matumizi ya mtindo unaohusiana na lugha katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

ii) Kubainisha matumizi ya mtindo yanayohusiana na vipengele vinginevyo vya kimtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

i) Ni matumizi gani ya kimtindo yanayohusiana na lugha yanayojitokeza katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*?

ii) Ni vipengele gani vingine vya kimtindo vinavyojitokeza katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa ni miongoni mwa tafiti za kwanza kwanza kushughulikia mtindo katika riwaya za watoto kwa kurejelea riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Kwa kuchambua matumizi ya mtindo katika riwaya hii kutawawezesha wahakiki na watafiti kwa jumla kuvifahamu vipengele vya mtindo vinavyounda riwaya ya watoto na pengine kulinganisha na kulinganua muundo wa riwaya za watoto na riwaya za wakubwa.

Utafiti huu pia utakuwa na umuhimu kwa watafiti na wanazuoni kufahamu namna mtindo ulivyo na mchango katika kukuza na kuendeleza dhamira katika riwaya za watoto na kuvutiwa kutafiti zaidi namna mtindo unavyohusiana na vipengele vingine vya kifani katika kuibua dhamira. Si hivyo tu, bali pia utafiti huu utahamasisha watunzi wengi zaidi kutunga riwaya kwa ajili ya watoto.

Utafiti huu pia utakuwa rejeleo la kutumainiwa katika uchunguzi wa fani ya riwaya utakaokuwa ukifanywa na watafiti wa baadaye. Kutokana na utafiti huu, watafiti wa baadaye wanaweza kuibua maarifa mapya ya kutafitiwa kwa lengo la kutimiza malengo yao ya utafiti na kuikuza zaidi taaluma ya riwaya.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unashughulikia matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kwa kuzingatia vipengele vya mtindo vya lugha na vipengele vingine vya

kimtindo kama vile mwingiliano wa tanzu, mwingiliano matini, wahusika na uteuzi wa visa na matukio. Edwin Semzaba ameandika kazi nyingi za tamthiliya na riwaya lakini *Marimba ya Majaliwa* ndiyo iliyotuvutia kuitafiti ili kuweza kutimiza malengo yetu ya utafiti.

## 1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii itakuwa na sura tano zilizokamilika. Sura ya kwanza imewasilisha vipengele vya utangulizi kama vile usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu. Sura ya pili imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu imewasilisha mbinu za utafiti kwa kuhusisha vipengele vya eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, data za msingi, data za upili, mbinu za kukusanya data; usomaji makini na upitiaji wa nyaraka, mbinu ya kuchambua data ya mkabala wa kimaelezo, kuzingatia maadili ya utafti na usahihi wa data. Sura ya nne imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti. Sura ya tano imewasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti zaidi katika siku zijazo.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia lengo likiwa ni kuweka bayana mambo ambayo tayari yameshafanyika kuhusiana na mada ya utafiti na nini bado hakijashughulikiwa. Sura hii ndiyo iliyosaidia kubaini pengo la maarifa ambalo ndilo limeshughulikiwa na sura hii. Pia, sura hii imeelezea nadharia ambayo imetumika katika kuchambua data za utafiti huu. Mambo yaliyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na ufafanuzi wa dhana muhimu katika utafiti huu, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, kazi tangulizi juu ya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*, mkabala wa kinadharia na pengo la maarifa.

## 2.2 Dhana ya Mtindo

Kwa kuwa utafiti wetu unachunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*, tumeona ni vizuri tufafanuwe dhana ya mtindo ili wasomaji waelewe tunamaanisha nini tunapoitumia dhana hiyo. Wamitila (2008) anaeleza kuwa mtindo ni elementi muhimu sana katika kazi za kifasihi. Ili kuweza kubainisha sifa za kimtindo za kazi ya kifasihi, mchanganuzi wa matini au kazi ya kifasihi anapaswa kuchunguza mambo mengi katika kazi inayohusika kama: uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mipangilio ya sentensi, uteuzi na matumizi ya tamathali za usemi na jazanda, usawiri wa wahusika, motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi, usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe na hata sifa za uakifishi hasa zinazoelekea kukiuka njia za kawaida za kuakifisha.

Ufafanuzi wa dhana ya mtindo unaotolewa na Wamitila (ameshatajwa) umesaidia kueleza sifa muhimu za mtindo ambazo hujitokeza katika kazi ya fasihi. Kama alivyosema kuwa mtindo unahusu mambo mengi naye hakuainisha yote lakini yale ya msingi ameyaainisha. Sifa nyingine za kimtindo ni namna ya uteuzi wa visa na matukio katika kazi ya fasihi, mwingiliano wa tanzu, mwingiliano matini na matumizi ya picha au michoro ambayo inafafanua juu ya maelezo yanayotolewa katika riwaya au kazi nyingine yoyote ya fasihi. Uelewa huu wa dhana ya mtindo iliyoelezwa na Wamitila (ameshatajwa) tumeuchukuwa na kuutumia katika utafiti wetu na wasomaji wetu pia waifahamu dhana hii kwa namna hii pale watakapokuwa wanaisoma kazi hii.

## 2.3 Fasihi ya Watoto

Utanzu wa fasihi ya watoto ni utanzu ambao umepuuzwa kwa miaka mingi katika maandishi ya kihakiki. Kazi nyingi za kihakiki hushughulikia fasihi ya watu wazima labda kutokana na imani ya kuwa fasihi ya watoto haistahiki kuchunguzwa kinadharia au inahusu tu ngano za chura na sungura. Fasihi ya watoto hurejelea matini au kazi ambazo kimsingi hadhira yake ni watoto (Wamitila, 2008).

Kwa kiasi kikubwa jinsi tunavyoziangalia matini au kazi hizo, yaani fasihi ya watoto yenyewe, huathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo au mawazo ya jamii kuwahusu watoto, yaani kile ambacho kinaweza kuelezwa kama itikadi ya jamii kuwahusu watoto. Itikadi hii inaathiri kwa kiasi kikubwa jinsi tunavyoteua kazi zenyewe za fasihi pamoja na matarajio tuliyonayo kuhusu kazi hizo: kuandikwa kwake, dhamira zake, wahusika wake, mwelekeo wake nakadhalika (Wamitila, 2008).

Fasihi ya watoto haitofautiani na fasihi nyingineyo katika sifa zake za kimsingi za kuwa sanaa ya lugha. Fasihi hiyo inaweza kuchunguzwa kwa utaalamu kwa kuukita uchunguzi huo katika misingi ya nadharia maalum. Wamitila anatueleza kuwa fasihi ya watoto ni kama fasihi nyingine na inaweza kuchunguzwa kwa kutumia nadharia za uhakiki wa fasihi. Marimba *ya Majaliwa* ni riwaya ya watoto na kwa maana hiyo ni fasihi ya watoto, nasi tumechunguza mtindo katika riwaya hiyo kwa kutumia nadharia ya Simiotiki.

## 2.4 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti

Mada ya utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Wapo wataalamu kadhaa ambao wameandika kuhusu mtindo katika riwaya mbalimbali na kwamba ni muhimu sisi kupitia kazi hizo kwa lengo la kupata hali halisi ya utafiti uliokwishafanyika kuhusiana na kipengele hiki. Mulokozi (1996) katika kazi yake ya utangulizi wa fasihi ametaja kipengele cha mtindo kama kipengele muhimu katika ujenzi wa kazi ya fasihi kama riwaya. Anaeleza kuwa mtindo ndio unaomtofautisha mtunzi mmoja na mwingine na kuwafanya wasomaji au wasikilizaji kusema kuwa wanaipenda kazi ya mtunzi fulani kuliko ya mtunzi mwingine.

Maelezo haya ya Mulokozi ni ya kweli hata katika nyimbo za muziki za mtunzi fulani huweza kupendwa na wasikilizaji zaidi kutokana na matumizi mazuri ya mtindo katika nyimbo za mtunzi huyo. Mawazo haya yamekuwa na manufaa kwetu kwa kutufanya tukawa makini katika kuchunguza ni vipengele gani vinavyoifanya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kuwa riwaya ya kipekee. Upekee wa riwaya hii

hutokana na matumizi ya mtindo yaliyotumiwa na mwandishi katika kuiandika riwaya hiyo. Kutokana na dhana kuwa mtindo ni upekee wa mwandishi katika kuiandika kazi yake, imetuwezesha kubaini matumizi ya mtindo kwa upana zaidi katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

Njogu na Chimerah (1999) katika kazi yao ya Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu, wameeleza namna mwandishi Shaaban Robert alivyokuwa bingwa wa matumizi ya mtindo ambao umekuwa ni rejeleo kwa watunzi wengine waliofuata baada yake. Wanaeleza kuwa Shaaban Robert katika utunzi wa riwaya zake amekuwa akitumia mtindo wa uteuzi wa wahusika bapa ambao hawabadiliki tangu mwanzo mpaka mwisho wa riwaya. Riwaya walizozitolea maelezo ni *Kusadikika* na *Kufikirika*. Katika riwaya hizi tunakutana na wahusika kama Karama na Majivuno ambapo Karama ni mhusika mwema na Majivuno ni mhusika mwenye maringo na mkandamizaji wa wanajamii. Shaaban Robert amekuwa akiwatumia wahusika wa aina hii kwa makusudi maalumu ya kuwataka wasomaji wake kujifunza kutokana na tabia za wahusika hao. Kwa jumla tunaweza kusema kuwa mtindo anaoutumia Shaaban Robert ni wa kimsisitizo ambapo anasisitiza mema yafanywe kupitia wahusika wema na maovu yasifanywe kupitia wahusika ambao ni waovu.

Maelezo ya Njogu na Chimerah (wameshatajwa) yametoa mchango muhimu katika kusukuma mbele utafiti baada ya kutufahamisha kwamba, matumizi ya mtindo wa wahusika wanaotumika katika riwaya za Shaaban Robert. Ingawa utunzi wa riwaya wa Shaaban Robert ni tofauti na utunzi wa riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* lakini mawazo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi. *Marimba ya Majaliwa* ni Riwaya

ya Watoto na riwaya za Shaaban Robert ni riwaya za watu wazima na vijana lakini riwaya hii pia imejengwa kwa wahusika na matukio ambayo ni ya kiuhalisiamazingaombwe kama zilivyo za Shaaban Robert. Kwa kulifahamu hili tumeweza kuelezea vizuri matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

Senkoro (2006) katika makala yake ya Makutano baina ya fasihi simulizi na andishi anaeleza kuwa kwa kiasi kikubwa fasihi andishi imechota vipengele vya kifasihi simulizi na kuvifanya kuwa ni vyake. Vipengele hivyo ni matumizi ya lugha, ujenzi wa wahusika, muundo, mtindo, mandhari, vichekesho na marudiorudio. Kwa asili vipengele hivi ni vya fasihi simulizi lakini leo vinatumika katika fasihi andishi katika kujenga dhamira kwa wasomaji wa kazi za riwaya, tamthiliya, hadithi fupi na ushairi. Maelezo haya kwa ujumla wake tunaweza kusema kwamba ni matumizi ya mtindo wa kifasihi simulizi ambao umechukuliwa na kutumika katika fasihi andishi. Mawazo haya yamefungua uelewa wetu kwamba hata katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kunaweza kuwa na mtindo wa kifasihi simulizi kwa kuwa ni riwaya andishi na hivyo kuwa imechota vipengele vya kifasihi simulizi. Jambo hili tulilitazama kwa kina katika utafiti huu kwa sababu limetupatia mawanda mapana zaidi ya kufahamu sifa za kimtindo katika kazi za fasihi na riwaya kwa jumla.

Naye Mohamed (2006) alitazama matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* iliyoandikwa na Shaaban Robert. Katika uchambuzi wake amebainisha mitindo mbalimbali inayojitokeza katika riwaya hiyo huku mtindo alioupa kipaumbele zaidi ni ule wa matumizi ya uwili kuwa ndio unaochukuwa nafasi kubwa

katika riwaya hii. Mtindo wa uwili unajitokeza pale mtunzi anaporejelea vitu kwa uwili uwili kama vile anapotaja dini ya Kiislamu atataja pia dini ya Kikiristo, akimtaja mwislamu anamtaja na mkiristo, akitaja msikiti anataja na kanisa, akimtaja mtu mwema anamtaja na muovu na akitaja umoja anataja na utengano. Matumizi ya mtindo huu yametokeza zaidi katika riwaya hii kuliko riwaya nyingine za Shaaban Robert kwa sababu dhamira kuu katika riwaya hii ilihitaji mtindo wa aina hii. Dhamira kuu katika riwaya hiyo ni haja ya dini zote kuungana na kuwa dini moja ambapo dini kuu ni Uislamu na Ukiristo. Shaaban Robert katika riwaya hiyo anaeleza kwamba, ikiwa nchi zinaweza kuungana na kuwa kitu kimoja kwa nini dini zisiungane? Kwa mtazamo wake ni jambo jepesi tu kwa dini kuweza kuungana na kuwa kitu kimoja ingawa kiuhalisia jambo hilo  ni gumu kwa sababu kila dini ina kanuni, sheria, taratibu, miongozo, mafunzo na imani ambayo ni tofauti na dini nyingine.

Mawazo haya yametusaidia kupata uelewa kwamba kuna uhusiano wa karibu baina ya mtindo na dhamira. Kama mtunzi anataka kuwasilisha dhamira fulani kwa hadhira yake lazima dhamira ihitaji mtindo wa aina fulani ili kuijenga vizuri dhamira hiyo. Katika tasinifu yetu tumechunguza namna mtindo ulivyosaidia kujenga dhamira zinazowahusu watoto katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

Wamitila (2008) ni mmoja kati ya wataalamu ambao wamechunguza matumizi ya mtindo katika kazi za riwaya. Katika kitabu chake cha kanzi ya fasihi ameelezea matumizi ya mtindo katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Shaaban Robert. Anaeleza kuwa, Shaaban Robert katika utunzi wake ana mwelekeo mkubwa wa

kutumia nathari ya kishairi na kutumia mashairi katika kazi zake za nathari. Pia ana matumizi ya majazi katika uteuzi wa majina, miundo ya uwili katika uendelezaji wa dhamira (wema hushinda ubaya), matumizi mapana sana ya tamathali za usemi na msamiati wa kiwango cha juu. Kezilahabi kwa upande mwingine yeye hutumia mtindo wa sentensi fupi fupi, matumizi ya lugha ya taswira, kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi-Kiingereza, Kilatini na Kiswahili. Pia mwandishi huyu ana mwelekeo mkubwa wa kuutumia ucheshi ambao unatokeza kwa namna tofauti kama matumizi ya majina, lugha na hali.

Mawazo haya ya Wamitila (ameshatajwa) yametusaidia kuelewa baadhi ya vipengele vya kimtindo vinavyotumiwa na watunzi wa riwaya maarufu kama Euphrase Kezilahabi na Shaaban Robert. Vipengele hivi tumevichunguza pia katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kwa lengo la kukamilisha lengo kuu la utafiti wetu.

Walibora (2010) alifanya utafiti na kufanikiwa kuandika makala juu ya Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe akilinganisha riwaya za *Dunia Yao* na *The Tin Drum*. Katika makala hayo alithibitisha kwamba riwaya hizi mbili zinafanana zaidi kuliko zinavyotofautiana katika kipengele cha mtindo ambapo mtindo wa kuelezea visa na matukio kuwa ni wa mambo yasiyoaminika kutokea katika ulimwengu halisi ndio ulichukuwa nafasi kubwa katika riwaya hizo. Matukio hayo ni kama vile mtu kuchapwa viboko na watu asiowaona, kusikia vicheko bila kuwaona wanaocheka, gari kupaa angani na mizumu kuzungumza na kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo. Mawazo haya ni mazuri na tumeyafanyia kazi katika tasinifu yetu ambapo tumeyachunguza matukio ya kiajabuajabu yaliyopo katika riwaya ya

*Marimba ya Majaliwa* kama mtindo wa kuwasilishia dhamira katika riwaya za watoto.

Onchangu (2013) alifanya utafiti na kuandika tasinifu yenye anuani isemayo "Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi." Katika tasinifu hii amebainisha kuwa pamoja na mambo mengine katika riwaya ya *Tumaini* na hadithi nyingine za Clara Momanyi matumizi ya mtindo wa lugha ya tamathali za usemi unajitokeza zaidi katika kazi hizo. Tamathali za usemi zinazojitokeza katika kazi hizo ni tashibiha, sitiari, tashihisi, jazanda na kadhalika. Mawazo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika tasinifu yetu. Ingawa riwaya ya Tumaini na Hadithi za Clara Momanyi zimeandikwa katika muktadha wa nchi ya Kenya lakini mtindo uliotumiwa na mwandishi katika utunzi wa kazi hizo una mchango katika kuelewa matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

Mwanzandi (2013) alifanya utafiti na kuandika makala juu ya Riwaya ya Karne ya 21 na Udurusu wa Nadharia za Fasihi. Pamoja na mambo mengine anaeleza kuwa riwaya zilizoandikwa katika karne ya 21 ni zile ambazo zimekuja na mtindo mpya kabisa wa uandishi ambapo visa na matukio mengi huwasilishwa kwa kurundikwa katika aya moja. Hii ina maana kwamba, mtunzi wa riwaya huandika riwaya yake kwa matukio na visa zaidi ya kimoja kuwekwa katika aya moja kiasi kwamba, kabla msomaji hajatafakari juu ya kile kinachoelezwa katika msitari wa kwanza, anakutana na kisa kingine katika msitari wa pili na kuendelea. Mtindo kama huu unahitaji msomaji ambaye ni makini na mzingativu ili aweze kuelewa dhamira zilizopo katika riwaya za aina hii. Msomaji ambaye si makini lakini pia si mtaalamu wa nadharia za

uhakiki wa fasihi hawezi kuielewa riwaya ya aina hii na mwishowe atatoa hitimisho kwamba riwaya za aina hiyo hazieleweki. Mawazo haya yamekuwa na mchango kwetu kuweza kufahamu kwamba kumbe tunaweza kutazama namna visa na matukio vilivyoshonana kama sehemu ya mtindo katika riwaya. Katika utafiti wetu tumetazama namna mshonano wa visa na matukio ulivyo katika *Riwaya ya Marimba ya Majaliwa* huku tukitambua kwamba hii ni riwaya ya watoto na si ya watu wazima.

## 2.5 Mapitio kuhusu Marimba ya Majaliwa

Kutokana na upya wa riwaya hii hakuna tafiti na tahakiki nyingi ambazo zimeshafanyika kuhusu riwaya hii. Kazi tangulizi kuhusu riwaya hii ni ile iliyoandikwa na Mulokozi (2008) katika Dibaji ya *Marimba ya Majaliwa* na Mwaijande (2012). Mulokozi (ameshatajwa) ameisifu riwaya hii kwa kupata tunzo ya kwanza katika mashindano ya mradi wa uandishi wa vitabu vya watoto yaliyoandaliwa na ubalozi wa Sweden nchini Tanzania. Mulokozi (2008:iv), anasema:

> *Marimba ya Majaliwa ni riwaya ya jusura. Jusura ni masaibu; ni matukio ya hatari na ya kusisimua yanayomsibu mtu, na yenye kuhitaji juhudi kubwa na ujasiri ili kuyashinda. Riwaya hii inahusu matukio ya namna hiyo yaliyomkuta kijana msanii, Majaliwa, katika harakati zake za kusaka marimba yake ya kimiujiza yaliyoporwa na msanii mwingine aitwaye Kongoti, na ambayo anayahitaji ili aweze kushinda mashindano ya kitaifa ya marimba. Katika msako huo wa kusisimua damu, Majaliwa anafanikiwa kuizunguka Tanzania nzima, na hivyo kumpeleka msomaji katika ziara ya kijiografia, kihistoria na kijamii ya nchi hii kubwa yenye kila aina ya utajiri na maliasili, nguvu kazi na simulizi za ushujaa uliotukuka. Tunaiona Tanzania kupitia macho ya Majaliwa na bibi yake kutoka kuzimu anayemsaidia katika mapambano.*

Maelezo haya ya Mulokozi yanaonyesha kwamba *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya yenye matumizi ya mtindo wenye vipengele vingi vya kuvutia. Katika utafiti huu

tumeyachukuwa mawazo ya Mulokozi na kuzamia kwa ndani ili kuibua matumizi ya mtindo katika riwaya hii ambayo imemwezesha mhusika Majaliwa kuzunguka Tanzania nzima.

Naye Mwaijande (2012) alichunguza dhima ya ucheshi katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* na kubainisha aina kadhaa za ucheshi. Katika maelezo yake anaeleza kuwa ucheshi katika *Marimba ya Majaliwa* unajitokeza zaidi kupitia uhalisia mazingaombwe ndani ya riwaya hiyo. Kauli hiyo ni ya kweli kwani ndani ya riwaya hiyo kumesheheni matukio ya kiuhalisia mazingaombwe pale ambapo Majaliwa akiingia tu katika hoteli na kutaka chakula basi hula chakula bila ya kulipa fedha na hushiba. Hii hutokea pale ambapo katika hoteli sharti kuwe na mtu ambaye amenunua chakula na anakula. Majaliwa akiingia hukiita chakula hicho na kuingia tumboni mwake na si katika tumbo la yule mnunuzi na mlaji halisi wa chakula hicho. Hiki kwa hakika si kitendo cha kawaida bali ni cha kiuhalisia mazingaombe. Mawazo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika tasinifu yetu ambapo tumebainisha aina kadhaa za mtindo ikiwemo uhalisia mazingaombwe kama unavyojitokeza katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

### 2.6 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia huelezwa kama kanuni, taratibu, miiko, muongozo au sheria zinazoelezea juu ya namna kitu fulani kilivyo au kinavyotakiwa kuwa. Katika maisha hakuna jambo linalofanywa bila kuongozwa na nadharia na hii ni sawa na kusema kuwa nadharia ndiyo inafanya jambo fulani lifanikiwe au lisifanikiwe. Ikiwa jambo limefanywa kwa kuzingatia nadharia vizuri jambo hilo litafanikiwa na ikiwa ni

kinyume chake jambo hilo haliwezi kufanikiwa. Kwa kuufahamu ukweli huu nadharia ya Simiotiki ndio itakayotumika katika kuchambua data za utafiti huu.

### 2.6.1 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni nadharia ya uhakiki wa mambo yanayohusiana na taaluma za lugha ikiwemo fasihi na isimu. Nadharia hii hushughulikia lugha ya misimbo na ishara kutokana na ukweli kwamba lugha huundwa na vitu viwili ambavyo ni kitaja na kitajwa (Mark, 1995). Kitaja ni maandishi yanayotumika kutaja kitu au mtu na hicho kitu au mtu ndio kitajwa yaani kinachorejelewa na jina hilo. Uzoefu unaonyesha kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa isipokuwa kwa baadhi ya maneno machache tu yenye sifa anomatopeiya (Eco, 1976). Maneno kama vile “nyau na pikipiki” yametokana na mlio unaotolewa na wahusika hawa ndipo wakapewa majina. Huu ni mfano wa majina ambayo yanaonekana kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kile kinachotajwa au kurejelewa lakini majina mengi hayana uhusiano kama huo.

Ni kutokana na hali hii ndio maana nadharia hii ikatajwa kuwa ni nadharia inayoshughulikia lugha ya picha na ishara kwa sababu watumiaji wa lugha huweza kutumia neno fulani lakini maana aliyoimaanisha ikawa si ile inayohusika na neno hilo. Taaluma ya fasihi ni sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa (Mlacha na Madumula, 1999). Ni lugha inayotumika katika kazi za fasihi ndiyo inayoifanya kazi husika kuwa sanaa na lugha hii si nyingine bali ni lugha ya picha, taswira, mafumbo, kejeli, ishara na jazanda. Kazi za fasihi simulizi na andishi zina matumizi ya lugha ya aina hii na ili kuweza kuelewa vizuri dhamira

zilizopo katika kazi hizo ni sharti msomaji awe na ujuzi wa nadharia kama hii. Malalamiko yanayotolewa na baadhi ya wasomaji kwamba, wanaposoma kazi fulani hawailewi ni kutokana na kutokuwa na maarifa ya nadharia kama hii.

Taaluma ya nadharia ya Simiotiki inaelekeza kwamba, matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi hujitokeza kwa kuzingatia misimbo kama mitano hivi ya nadharia hii. Misimbo hiyo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihemenitiki, msimbo wa kiseme, msimbo wa kiutamaduni na msimbo wa kiurejelezi. Msimbo wa kimatukio unahusu uelezewaji na uwasilishwaji wa matukio katika kazi ya fasihi. Kwa mfano, mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kuwasilisha tukio fulani katika kazi yake kwa kutumia picha au taswira na kuiwasilisha kwa wasomaji wake. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Mashetani* (1972) iliyoandikwa na Ebrahim Hussein kuna tukio la mhusika shetani kumpatia mhusika binadamu kisu na kisha binadamu kuamriwa amchinje shetani na yeye shetani mwenyewe. Hili tunasema ni tukio la kimsimbo kwamba kuna picha fulani inajengwa hapo tofauti na vile ilivyoandikwa au kuelezewa. Hili ni tukio la wakoloni kuzipatia nchi za Kiafrika uhuru lakini kumbe ni uhuru wa bendera tu. Hii ina maana kwamba, nchi za Afrika tayari zimeshapewa uhuru lakini haziwezi kuutumia uhuru huo kufanya maamuzi yao bila kuongozwa na nchi zilizoendelea ambazo ndizo ziliitawala Afrika enzi hizo. Kwa hiyo, mtaalamu wa nadhari hii anapokutana na tukio kama hili mara moja hutambua dhamira inayowasilishwa katika tukio la kimsimbo kama hili.

Aina nyingine ya msimbo katika nadharia ya Simiotiki ni msimbo wa Kihemenitiki. Huu ni msimbo ambao unahusu anuani ya kifasihi kama vile jina la kitabu, jina la

mchezo wa kuigiza, kichwa cha shairi na kadhalika. Majina mengi ya kazi za fasihi hubuniwa kimsimbo, yaani unapolisoma jina hilo unaanza kupata dhana kwamba katika riwaya, tamthiliya, mashairi au hadithi hii kutakuwa kunazungumzwa dhamira za aina fulani. Jina la kitabu linatosha kumfahamisha msomaji yaliyomo ndani ya kitabu hicho kabla hata hajafungua na kuanza kusoma kitabu hicho. Msimbo huu wa Kihemenitiki ni mzuri kwa sababu humwezesha msomaji kuamua kusoma au kutosoma kitabu baada ya kuona jina la kitabu hicho na kupata dokezo la yale yanayozungumzwa katika kitabu hicho.

Msimbo wa kiutamaduni nao ni moja kati ya misimbo ya nadharia ya Simiotiki ambapo watunzi wa kazi za fasihi hutumia viashiria na mambo ya kiutamaduni kuelezea dhamira ambayo anataka hadhira iipate. Kwa mfano, mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kuwa anataka kuelezea hali ya maisha halisi ya jamii fulani na hapo atatumia viashiria vya kiutamaduni kama mavazi ya jamii hiyo, nyumba zao, shughuli zao za kimila na desturi. Msomaji au mhakiki ambaye ni makini anaweza kuibua dhamira mbalimbali kutokana na viashiria hivyo vya kiutamaduni. Mathalani, nyumba za msonge ni moja kati ya vitu vya kiutamaduni katika jamii nyingi za Kiafrika na nchi ya Tanzania ikiwepo. Hata hivyo, ujenzi wa nyumba za siku hizi ni za kisasa zaidi kuliko nyumba za msonge. Mwandishi anapotaja nyumba za aina hii katika kazi yake hujenga msimbo wa kiutamaduni juu ya dhamira ya umasikini katika jamii.

Msimbo wa kiseme hufahamika kama msimbo unaojenga dhamira kwa kurejelea maana za maneno kwa kuzihusisha na maana ya msingi ya maneno hayo. Kwa

mfano, mtunzi anaweza akamtumia mnyama simba katika kujenga sitiari kama vile Mwakipesile ni Simba. Katika hali ya kawaida Mwakipesile hawezi kuwa simba ila anaweza kuwa ni mtu mkali sana kama simba. Hapa tumechukua maana ya msingi ya neno simba ambayo ni mnyama mkali wa mwituni aliye hatari kwa maisha ya wanyama wengine na binadamu pia. Kwa maana hiyo, Mwakipesile ni mtu mkali na haitakiwi kumchezea au kumuudhi kwa namna yoyote ile.

Msimbo wa mwisho katika mtiririko wa maelezo yetu ni msimbo wa kiurejelezi. Mtunzi wa kazi ya fasihi huutumia msimbo huu pale anapotumia kitu fulani kurejelea kitu kingine ambacho kimaana kinakaribiana na hicho kinachoelezewa. Mfano mzuri ni usemi huu, "paka haishi kwa msela," ikiwa na maana kwamba mnyama paka ambaye hufugwa nyumbani hawezi kuishi katika nyumba inayokaliwa na mtu ambaye huwa hapiki chakula nyumbani kwake. Vijana ambao hawajaoa wengi wao huwa hawapiki chakula mahali wanapoishi bali hununua chakula katika migahawa na kula hukohuko. Paka ambaye hutegemea kupatiwa chakula kinachopikwa nyumbani hawezi kuishi mahali hapo kwa sababu atakosa chakula. Msemo huu kimsingi umetumika kiurejelezi kwamba hakuna mtu ambaye anaweza kuishi mahali ambapo hakuna chakula au mahitaji muhimu kwa maisha ya mtu. Ikiwa kijana amefikisha umri wa kuoa na kuamua kuoa halafu ikawa hakuna chakula nyumbani kwake ni wazi mke ataondoka mahali hapo na kurudi kwao.

Kimsingi, nadharia ya Simiotiki imekuwa na msaada mkubwa katika kuchambua data za utafiti huu kwa ufanisi mkubwa. Misimbo yote mitano imetuwezesha

kubainisha matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kwa kutupatia aina za mitindo ambazo hatukutaraji kupata katika riwaya hii.

## 2.7 Pengo la Maarifa

Mapitio ya kazi tangulizi yanaonyesha kuwa watafiti watangulizi wameshughulikia kipengele cha mtindo katika riwaya za watu wazima huku zile za watoto kama *Marimba ya Majaliwa* zikiwekwa pembeni. Hivyo, tuliona kwamba ipo haja ya msingi ya kuziba pengo hili la maarifa kwa kuchunguza mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia kwa lengo la kubainisha pengo la maarifa. Katika sura hii tumefanikiwa kuwasilisha ufafanuzi wa dhana za mtindo na fasihi ya watoto. Tuliona kwamba ipo haja ya msingi ya kufafanua dhana hizi ili msomaji atakapokutana nazo mara kwa mara katika tasinifu hii asibabaike na kujiuliza maana yake ni nini? Pia, tumepitia kazi tangulizi zilizofanywa kuhusiana na mada ya utafiti ambapo kazi mbalimbali zimepitiwa na kubaini kwamba hakuna mtafiti mtangulizi yeyote aliyechunguza mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Mkabala wa kinadharia pia umewasilishwa katika sura hii ambapo nadharia ya Simiotiki pamoja na misimbo yake mitano imeelezewa kwa kina na kuonyesha namna inavyojitokeza katika kazi za fasihi.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha mbinu za utafiti za kukusanya na kuchambua data. Mbinu za utafiti ndizo ambazo hutumika katika kukusanya na kuchambua data kitaalamu na kisayansi ili kuufanya utafiti uaminiwe. Utafiti wowote ambao unafanywa bila ya kuwa na mbinu za utafiti zinazokubalika kulingana na malengo ya utafiti, utafiti huo utakuwa ni batili na hauwezi kuaminiwa katika tasinia ya taaluma husika. Sura hii imewasilisha eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, aina ya utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data; usomaji makini na upitiaji wa nyaraka, mbinu za uchambuzi wa data; mkabala wa kimaelezo, usahihi wa data za utafiti na maadili ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti umefanyika kwa maana ya kukusanya data na kuzichambua (Cohen, 2000). Eneo la utafiti huteuliwa kwa malengo kwamba eneo hilo litamwezesha mtafiti kupata data zinazotakiwa kutimiza lengo kuu la utafiti husika. Eneo la utafiti huu lilikuwa ni Dar es Salaam na Iringa. Mkoa wa Dar es Saalam uliteuliwa kwa sababu kunapatikana maktaba ambazo zina machapisho na maandiko ambayo yanahusiana na mada ya utafiti. Maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Mkoa wa Iringa uliteuliwa kwa sababu ndipo mahali ambapo mtafiti anaishi na aliweza kukusanya data za msingi akiwa Iringa katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria

Cha Tanzania kituo cha mkoa wa Iringa. Data za msingi zilikusanywa katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ambapo mtafiti alikaa kwa utulivu katika maktaba hiyo na kusoma kwa makini riwaya hiyo kwa lengo la kupata data zenye matumizi ya mtindo ndani ya *Marimba ya Majaliwa*.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti ni jambo la kitaalamu ambalo linahitaji kufanywa kwa kuzingatia taratibu maalumu za kiutafiti. Usanifu wa utafiti ni muongozo unaoeleza namna utafiti utakavyofanywa, utafiti huo utakuwa ni wa namna gani na data zitakusanywa kwa kutumia mbinu gani? Usanifu wa utafiti ni maelezo yanayotolewa kuelezea muundo au umbo la utafiti husika tangu katika kusanya data, kuchambua na kuandika tasinifu (Kombo na Tromph, 2006). Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani unaohusu kuteuliwa kwa eneo au jambo maalumu ambalo ndilo hushughukiwa kindakindaki na kupatiwa majibu stahiki (Kothari, 2008). Katika tasinifu hii riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ndiyo iliyoteuliwa kama uchunguzi kifani ambapo matumizi ya mtindo katika riwaya hiyo ndiyo yaliyotafitiwa. Uchunguzi kifani ni aina nzuri ya usanifu wa utafiti kwa sababu humrahisishia mtafiti shughuli zote za utafiti kwa kuzifanya kwa ufanisi bila kupoteza muda. Mtafiti hawezi kupoteza muda wake kwa sababu tayari ameshajuwa jambo analolitafiti na hivyo atalimakinikia jambo hilo.

### 3.4 Aina ya Utafiti

Kimsingi, kuna aina kuu mbili za utafiti ambazo ni utafiti wa uwandani na utafiti wa maktabani. Utafiti wa uwandani ni ule unaohusisha kukusanya data kutoka katika makazi moja kwa moja kwa kuwasaili au kuwahoji watafitiwa waliolengwa katika

utafiti huo (Babbie, 1999). Utafiti wa maktabani ni ule ambao unahusisha kukusanya data kutoka katika maktaba kwa kusoma kazi tangulizi au kazi maalumu iliyoteuliwa kama ni utafiti unaohusisha fasihi andishi kama hii (Robson, 2007). Utafiti wetu ulikuwa ni wa maktabani kwa asilimia mia moja ambapo data za msingi za utafiti zimekusanywa kutoka katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Data zilizokusanywa kutoka katika riwaya hii ni zile zinazohusiana na matumizi ya mtindo katika riwaya hii ambayo kwa asili ni riwaya ya watoto iliyowahi kupata tunzo ya kwanza katika mashindano ya utunzi wa vitabu vya watoto.

## 3.5 Kundi Lengwa

Kundi lengwa hurejelea walengwa ambao watahusika katika kutoa data za utafiti kwa lengo la kutimiza lengo kuu la utafiti (Yin, 2001). Kundi lengwa katika utafiti huu ni riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ya mwandishi na mwalimu maarufu wa fani za uigizaji na hadithi za kubuni Edwin Semzaba. Kilicholengwa kushughulikiwa katika riwaya hii ni matumizi ya mtindo na namna mtindo ulivyosaidia kuunda dhamira katika riwaya hiyo.

## 3.6 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni kile ambacho kimeteuliwa kuwa kiwakilishi cha watafitiwa wote wanaohusika katika utafiti husika (Young, 1984). Katika hali ya kawaida hakuna utafiti makini ambao unaweza kufanywa kwa kushirikisha watafitiwa wote wanaopatikana katika jamii au taifa fulani. Upo ulazima wa kuteua sehemu kutoka katika jamii hiyo ili kupata sampuli ya kufanyiwa utafiti. Sampuli ya utafiti huu ni riwaya moja ya *Marimba ya Majaliwa* ya mwandishi Edwin Semzaba. Zipo riwaya

na kazi nyingine kadhaa za mwandishi Edwin Semzaba lakini katika utafiti huu tumeteua riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kama sampuli ya utafiti wetu ili kutimiza lengo kuu la utafiti huu.

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sampuli ambayo imetumika katika kutoa data za utafiti husika. Zipo mbinu tofautitofauti za usampulishaji ambapo katika utafiti huu tulitumia mbinu ya usampulishaji lengwa kuteua riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Usampulishaji lengwa ni mbinu ya kuteua sampuli kwa makusudi kwanza sampuli ambayo mtafiti ana uhakika kuwa itampatia data ambazo zitajibu maswali ya utafiti wake. *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya ambayo imeteuliwa kwa makusudi kuwa ndiyo ambayo inaweza kutoa data muafaka za kukamilisha malengo ya utafiti huu.

## 3.7 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti huu umekusanya data za msingi na upili kupitia vyanzo kadhaa kama vilivyoainishwa katika sehemu ifuatayo:

### 3.7.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo ndio kwanza zimekusanywa kwa mara ya kwanza kabisa na kuwasilishwa katika ulimwengu wa taaluma (Kothari, 2008). Data hizi hukusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji, majadiliano ya kikundi lengwa, ushuhudiaji, ushiriki na usomaji makini. Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini katika riwaya ya Marimba ya Majaliwa. Riwaya hii imesomwa kwa makini na kukusanya data zinazohusiana na matumizi ya mtindo katika riwaya hii kama mada ya utafiti ilivyoelekeza.

### 3.7.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo zinakusanywa kutoka katika machapisho na maandiko ambayo tayari yapo katika maktaba (Yin, 2001). Data hizi hukusanywa kwa lengo la kujazilishia au kukazia maarifa yaliyopatikana kutokana na data za msingi. Wataalamu wa mbinu za utafiti huiita mbinu hii kama ni ya kukusanyia data za utafiti mezani. Data za upili katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## 3.8 Ukusanyaji wa Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani.

### 3.8.1 Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi zinazohusiana na taaluma ya fasihi pamoja na masuala ya lugha. Mbinu hii hutumika kukusanya data kwa mtafiti kusoma kwa makini kazi iliyolengwa kutoa data za utafiti na kudondoa data hizo katika shajara maalumu lililoandaliwa kwa ajili ya kazi hiyo (Kombo na Tromph, 2006). *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya ambayo imesomwa kwa makini na kufanikisha kukusanya data za msingi za utafiti.

Data za msingi zilizotakiwa katika utafiti huu ni zile za matumizi ya mtindo katika riwaya hii ambapo mtafiti aliandaa utaratibu maalumu wa kukusanya data za utafiti. Kwanza tuliandaa shajara ambalo liligawanywa katika sehemu mbili; sehemu ya

kwanza iliwekwa mada ambazo zinausiana na lengo mahususi la kwanza, sehemu ya pili ni mada zinazohusiana na lengo mahususi la pili la utafiti.

Mtafiti alisoma riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* zaidi ya mara tano kabla ya kuanza kudondoa data katika shajara na ilipofika mara ya sita ndipo alipoanza kukusanya data kwa kudondoa na kuandika katika sehemu maalumu iliyoandaliwa katika shajara. Mtafiti alisoma riwaya husika mara nyingi zaidi na kukusanya data mpaka alipofikia nahali pa kupata za kutosha ndipo alipoanza kuzipanga data hizo kwa namna ambayo ni rahisi zaidi ya kufanyia uchambuzi.

### 3.8.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kwani kupitia nyaraka zinazohusiana na mada ya utafiti katika maktaba ili kupata za kukazia au kushadadia hoja zinazoibuliwa na data za msingi (Cresswell, 2009). Upitiaji wa nyaraka husaidia kupatikana kwa data ambazo kimsingi humuongoza mtafiti katika kuandika mambo yenye mantiki kwa sababu mtafiti anaona namna wenzake walivyoandika na yeye hawezi kwenda mbali nao.

Nyaraka zilizopitiwa katika utafiti huu ni zile ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusiana na mada ya utafiti kama zilivyowasilishwa katika sura zote za tasinifu hii. Katika kila sura ya utafiti huu tumetumia mawazo ya wataalamu tofautitofauti ambao tumesoma kazi zao kupitia mbinu hii ya upitiaji wa nyaraka. Nyaraka hizo tumezisoma katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## 3.9 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kutolea ufafanuzi data zilizokusanywa kwa namna ambayo inasaidia kujibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo ya utafiti. Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa Kimaelezo.

### 3.9.1 Mkabala wa Kimaelezo

Utafiti unaohusiana na taaluma za fasihi mara nyingi huchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kwa sababu fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ili kuichambua lugha hiyo lazima kuwe na mkabala wa kimaelezo. Hii haina maana kuwa data za taaluma ya fasihi huwa hazichambuliwi kwa kutumia mkabala wa kimahesabu. Mkabala wa kimahesabu huweza kutumika kulingana na mada na malengo ya utafiti husika. Katika utafiti huu data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo ambapo maelezo muafaka yametolewa kwa kila dondoo lililowasishwa katika sura ya nne ya tasinifu hii. Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data za utafiti kwa mtafiti kutolea maelezo data hizo huku zikishadidiwa na maelezo kutoka katika nadharia na kazi tangulizi (Cresswell, 2009).

## 3.10 Usahihi wa Data za Utafiti

Data za utafiti huu ni sahihi kwa sababu zimekusanywa kwa kuzingatia kanuni na taratibu zote za ukusanyaji wa data katika utafiti. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Mbinu hizi mbili ni madhubuti na muafaka katika kusaidia kupatikana data za kifasihi kama ilivyo kwa utafiti wetu. Mapungufu ya mbinu ya usomaji makini yamedhibitiwa na mbinu ya

upitiaji wa nyaraka na yale ya upitiaji wa nyaraka nayo yamedhibitiwa na usomaji makini na hivyo kupata data ambazo ni sahihi.

### 3.11 Maadili ya Utafiti

Hakuna jambo ambalo linaweza kufanywa bila kuwa na maadili ya kuongoza namna jambo hilo linavyotakiwa kufanywa ili litoe tija kwa wahusika. Utafiti nao hufanywa kwa kuzingatia maadili ya kiutafiti (Babbie, 1999). Katika utafiti huu tulihakikisha kwamba data tulizokusanya zinatoka katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* tuliyoiteua kuifanyia utafiti. Data hizo zilidondolewa kutoka katika riwaya hiyo kwa makini bila kukosea ili kuwa na data za uhakika na zinazoaminika.

### 3.12 Hitimisho

Sura hii ya tatu ya tasinifu hii imewasilisha mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Mambo yaliyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, aina ya utafiti, kundi lengwa na sampuli na usampulishaji. Mbinu nyingine ni aina ya data zilizokusanywa; data za msingi na upili, mbinu za kukusanyia data; usomaji makini na upitiaji wa nyaraka, mbinu za uchambuzi wa data; mkabala wa kimaelezo, usahihi wa data na maadili ya utafiti.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Lendo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* (2008). Ili kutimiza lengo hili, malengo mahususi mawili yaliandaliwa ambayo yalikuwa ni kubainisha matumizi ya mtindo yanayohusiana na lugha katika riwaya teule na kubainisha matumizi ya mtindo kwa kurejelea vipengele vingine vya kimtindo katika riwaya teule. Hivyo, sura hii ya nne ya tasnifu imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa kutumia malengo hayo mawili ya utafiti. Hii imesaidia kuiwezesha sura hii kutimiza lengo kuu la tasinifu hii kwa ufanisi.

## 4.2 Matumizi ya Vipengele vya Lugha vya Kimtindo

Mtindo unaelezwa kuwa ni jinsi au namna ambavyo mwandishi wa kazi ya fasihi anavyoiwasilisha kazi yake kwa hadhira ikiwa ni tofauti na waandishi wengine (Mlacha, 1996). Hii ni sawa na kusema kuwa, mtindo humtofautisha mwandishi mmoja na mwingine na hujitokeza pale ambapo hadhira hueleza bayana kuwa wanaipenda kazi ya mtunzi fulani kuliko mtunzi au watunzi fulani. Mtindo katika kazi ya sanaa hujitokeza katika vipengele mbalimbali lakini kipengele cha matumizi ya lugha huchukuwa nafasi kubwa katika mtindo uliojenga kazi ya fasihi. Hii imetufanya kuwa na lengo mahususi moja ambalo linashughulikia matumizi ya mtindo wa lugha katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Kwa kuwa vipengele vya mtindo vya lugha ni vingi tumeteua baadhi tu ya vipengele ili kutimiza malengo ya

utafiti. Miongoni mwa vipengele hivyo ni pamoja na:

### 4.2.1 Matumizi ya Tashibiha

Tashibiha ni moja kati ya vipengele vya tamathali za usemi ambacho hutumika katika kufananisha vitu viwili ambavyo havina sifa za kufanana kuwa vinafanana bila ya kuwa na tofauti yoyote. Tashibiha hutumia viunganishi linganishi ambavyo ni kama, kama vile, sawasawa na, sawasawa kabisa na, mithili ya, mfano wa na kadhalika (Madumullah, 2009). Tashibiha ni kipengele maarufu katika fasihi simulizi kutokana na kujitokeza kwake karibu katika kila utanzu wa fasihi hiyo. Vilevile, hata katika fasihi andishi pia tashibiha hujitokeza mara nyingi kwa malengo ya kufikisha ujumbe kwa hadhira. Kipengele hiki tumekiita kuwa ni sehemu ya matumizi ya mtindo kwa sababu kila mwandishi ana namna yake ya kuzijenga tashibiha ndani ya kazi yake tofauti na mwandishi mwingine. Edwin Semzaba ni mmoja kati ya waandishi ambaye ametumia tashibiha katika utunzi wake wa riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> *Majaliwa aliimba huku akifanya kazi kwa nguvu. Watu wakamkodolea macho, wakishangazwa na umahiri wake wa kuimba. Alisikia mmoja wao akiuliza, "Kwa nini asingeingia kwenye mashindano ya kuimba huko mjini?" Na mwingine akaongeza, "Huyu ni manju haswa," kisha akaongeza, "Hawa ndio Siti Binti Saad hawa. Waimba kama chiriku. Siti alianza kuimba wakati akiuza vitumbua, mpaka akaja kuwa mwimbaji mashuhuri, Unguja haijapata kuona!" (uk. 11).*

Katika dondoo hili kuna matumizi ya tashibiha ambapo uwezo wa Majaliwa wa kuimba unafananishwa sawa na ule wa chiriku. Chiriku ni jamii ya ndege ambao huimba nyimbo mbalimbali mfululizo bila ya kupumzika. Nyimbo hizo huimbwa kwa mpangilio mzuri kiasi cha kumfanya msikilizaji kuvutiwa na nyimbo hizo na

kisha kuwa makini kuzisikiliza. Mwandishi anamsifu Majaliwa kuwa naye anaweza kuimba sana kama asemavyo, "waimba kama chiriku." Hii ni tashibiha inayoonyesha namna Majaliwa alivyokuwa na kipaji cha kuimba ndio maana hata katika msitari wa mwisho tunaona uimbaji wake ukifananishwa na ule wa Siti Binti Saad. Huyu alikuwa ni mwimbaji maarufu wa taarab katika Afrika na ulimwenguni, aliyesifika kwa sauti yake nzuri ya kumtoa nyoka pangoni. Matumizi ya tashibiha kama hii ni mazuri katika riwaya za watoto kama hii ya *Marimba ya Majaliwa* kwa sababu humfanya mtoto aelewe vizuri dhamira za riwaya hii. Watoto hupenda ndege warukao angani na hata wale wafugwao nyumbani, hivyo kutumia ndege kama sehemu ya tashibiha ni ubunifu wa mtunzi ambao unaonyesha upekee wake wa matumizi ya mtindo katika riwaya yake.

Kutokana na nafasi ya mtindo wa tashibiha katika kuifanya hadhira ielewe kazi husika, mtafiti amekuwa akiutumia mtindo huu katika sehemu nyingi za kazi yake. Dondoo lifuatalo linaendelea kuthibitisha:

> *Alifika stendi huku akihema kama jogoo aliyetoka kupigana. Mabasi yalikuwa mengi. Aliingia ndani ya kila basi, bila kujali lilikuwa la wapi na kuchungulia. Hakumwona Kongoti. "Kuna basi liendalo Moshi liliondoka karibuni?" Majaliwa alimuuliza mmoja wa vijana wanaotembeza matunda.*
>
> *"Hapana. Basi la mwisho kuondoka lilikuwa Ubuyu Wangu, saa moja iliyopita." Majaliwa alishangaa* (uk. 44).

Katika dondoo hili kuna matumizi ya tashibiha, "alifika stendi huku akihema kama jogoo aliyetoka kupigana." Matumizi haya ya tashibiha yanaonyesha kuwa Majaliwa alikimbia umbali mrefu kwa kasi bila hata ya kupumzika ndio maana alikuwa akihema kama jogoo. Hapa tena tunaona namna mwandishi akirejelea mtindo wake

wa matumizi ya tashibiha ambayo inahusisha ndege aina ya kuku ambaye ni jogoo. Jogoo ni aina ya ndege ambaye hufugwa nyumbani na watoto hucheza naye katika michezo yao kila siku. Kutumiwa kwa jogoo katika tashibiha hii kuna thibitisha kwamba *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya ya watoto kwani inatumia vitu vinavyomzunguka mtoto katika mazingira yake anamoishi.

Kimsingi, matumizi ya tashibiha tuliyoyabainisha hapo juu yanaonekana kuwa yamejengwa kwa kutumia nadharia ya Simiotiki. Jongoo na Chiriku wametumika kiishara kuonyesha kuwa ni ndege wenye uwezo mkubwa wa kufanya vitu ambavyo ni vya kishujaa na vya kusifiwa (Cobley, 2001). Mtoto mdogo anapoisoma riwaya hii anajifunza kuwa shujaa kwa kutaka kuwa kama jogoo au kuimba vizuri kama chiriku. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba kwa matumizi ya mtindo huu mwandishi amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuifanya riwaya yake kuwa ni riwaya ya watoto.

### 4.2.2 Matumizi ya Chuku

Chuku ni moja kati ya vipengele vya matumizi ya lugha ambapo mtunzi hutumia lugha iliyotiwa chumvi katika kuelezea jambo fulani ndani ya kazi yake. Katika uhalisia wa maisha, kuna mambo ambayo yanafahamika moja kwa moja kuwa utokeaji wake ni wa aina fulani iliyozoeleka na kila mtu hutaraji kuliona hilo. Hata hivyo yapo mazingira ambayo jambo huelezwa kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Mwandishi Edwin Semzaba ametumia mtindo wa lugha ya chuku mahali pengi katika kazi yake. Dondoo lifuatalo linathibitisha matumizi ya chuku katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*:

> *Vile vibwengo, idadi yao kama mia mbili, vikawazunguka. Bibi akatoa pumzi chafu kwa nguvu, sauti yake kama mzinga. Basi, vile vibwengo vyote vikakimbia na kutawanyika huku vimekamata pua zao. Harufu ya hewa chafu ilikuwa komesha. Majaliwa hakuweza kuipata kwa sababu ya kinga ya bibi yake. "Mjukuu wangu Majaliwa umeona mwenyewe?" Bibi aliuliza.*
>
> *Nimeona bibi. Hivyo hawatarudi tena?" Majaliwa aliuliza. "Thubutu!" Bibi alimjibu. "Ile harufu ni kwa kuwa wewe hukuinusa. Haina mchezo. Nikiitoa kwa binadamu watazimia kwa siku tatu. "Siku tatu!" Au zaidi!...* (uk. 26).

Dondoo hili limetumia matumizi ya lugha ya chuku kuhusu pumzi chafu au ushuzi ambao hutolewa na binadamu. Mwanadamu ni kiumbe ambaye hutoa hewa chafu kama sehemu ya mfumo wa uhai wa maisha yake. Hivyo, kutoa hewa chafu ni kitendo cha kawaida, lakini pale tunapoelezwa kuwa hewa hiyo hiyo chafu ambayo inatoka kwa mwanadamu inaweza kuwafanya wanadamu wakazimia kwa siku tatu hapo ndipo tunapoyaona vizuri matumizi ya mtindo wa lugha ya chuku. Katika hali ya kawaida hakuna hewa chafu au ushuzi kutoka kwa binadamu ambao unaweza kusababisha watu wengine wazimie. Ila ni sahihi kusema kuwa, upo uwezekano wa mtu kutoa hewa chafu ambayo itawafanya watu washindwe kukaa mahali hapo lakini si kwamba watazimia. Matumizi ya lugha ya aina hii ni muafaka kwa vitabu vya watoto kama ilivyo *Marimba ya Majaliwa*. Hii huwafanya watoto kujenga imani kwamba mtu mwenye uwezo wa kuwafanya watu wakazimia kwa kutumia ushuzi ni mtu ambaye anapaswa kuheshimiwa kwani hakuna kitu katika maisha ambacho anashindwa kukifanya. Mtu wa aina hii husikilizwa sana na watoto na kila anachosema huchukuliwa kwa uzito mkubwa. Hivyo, matumizi ya chuku katika dondoo hili hayakufanywa kwa bahati mbaya bali kwa sababu maalumu ya kujenga imani na utii kwa watoto ambao ndio walengwa wa riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

Katika kuthibitisha kuwa *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya ya watoto kuna matumizi mengi ya mtindo wa lugha ya chuku. Dondoo lifuatalo ni mfano maridhawa:

> *Majaliwa alijikuta akiwa pamoja na samaki wakiingia kwa kasi kwenye kinywa kikubwa cha nyangumi. Nyangumi alipofungua mdomo, ukubwa wake ulikuwa kama kontena mbili kwa pamoja. Tumbo lake lilikuwa kubwa na lenye kuweza kuingiza makontena kumi kwa wakati mmoja! Ndani ya tumbo kulikuwa na giza lililozidi lile la baharini, lakini joto lilikuwa kidogo. Majaliwa hakuwa na wasiwasi kwani aliendelea kuvuta pumzi kama kawaida. Alitupa macho huko na huko, akashangazwa na matumbo yaliyokuwa makubwa na marefu sana. Majaliwa aliona pia mayai ambayo yalikuwa yakiendelea kutengenezwa. Akayasogelea kwa shauku.*
>
> *Mayai ya nyangumi yalikuwa makubwa kama magunia yaliyojaa mchele* (uk. 37).

Katika dondoo hili tunaendelea kubaini matumizi ya mtindo wa lugha ya chuku. Anatajwa samaki aina ya nyangumi ambaye anasifika kuwa ni mmoja kati ya samaki wakubwa katika jamii ya samaki baharini. Hata hivyo, sifa anazopewa samaki huyo katika dondoo hapo juu zinaonyesha bayana kuwa zimetiwa chumvi ili kumfanya msomaji ambaye ni mtoto kuelewa kwamba yupo samaki mkubwa kuliko wote baharini. Matumizi haya ya lugha ya chuku yamejengwa kwa kutumia msimbo wa kimatukio ambayo katika uhalisia hayawezi kutokea lakini kwa ulimwengu wa lugha ya chuku yanatokea. Tunaelezwa kuwa Majaliwa naye aliingia katika tumbo la nyangumi na akawa anaweza kuvuta hewa kama vile yupo katika mazingira ya kawaida. Kiuhalisia tunafahamu kuwa binadamu anaweza kuvuta hewa pale anapokuwa katika ulimwengu halisi na si katika bahari tena ndani ya tumbo la samaki aina ya nyangumi. Matumizi ya chuku za aina hii humfanya mtoto ambaye ndiye mlengwa wa riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kuwa na uwezo wa kufikiri zaidi juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maisha (Mulokozi, 2008).

### 4.2.3 Matumizi ya Takriri

Takriri ni moja kati ya vipengele vya matumizi ya lugha katika kazi za fasihi ambapo kunakuwa na marudiorudio ya herufi, silabi, neno, sentensi na wakati mwingine hata aya nzima hurudiwa (Msokile, 1993). Watunzi wa kazi za fasihi hutumia mtindo wa kurudiarudia vipengele tulivyovitaja kwa sababu maalumu ambayo ni kumtaka msomaji au msikilizaji kuwa makini juu ya kile kinachoelezwa. Katika *Marimba ya Majaliwa* kuna matumizi mengi ya takriri kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> *Usiku ule Majaliwa hakupata usingizi. Kila mara aliimba wimbo huu mpaka alipopata usingizi:*
> *"Nasikitika mubaraka, nasikitika mubaraka*
> *Marimba yangu kuibiwa, nasikitika mubaraka*
> *Nasononeka moyoni, nasononeka mubaraka*
> *Marimba yangu kuibiwa, nasononeka mubaraka."*
> *Alipokuwa amelala, marehemu bibi yake mzaa mama, alimjia ndotoni na kumwambia, "Mjukuu wangu, Majaliwa, Kongoti Nachienga ndiye ameiba marimba yako. Ana wasiwasi utamshinda huko Dodoma* (uk. 03).

Tunapolitazama dondoo tajwa hapo juu, tunabaini kuwa kuna matumizi ya mtindo wa lugha ya takriri wa kipekee. Kwanza, kuna takriri neno ambapo maneno kadhaa yamerudiwa, mathalani, neno "mubaraka," limerudiwa mara tano, neno "nasikitika," limerudiwa mara tatu na neno "nasononeka," nalo limerudiwa mara tatu. Pili, kuna marudio ya sentensi ambapo sentensi "nasikitika mubaraka," imerudiwa mara tatu na sentensi "nasononeka mubaraka," imerudiwa mara mbili. Matumizi ya mtindo wa aina hii yanamfanya msomaji kuwa makini katika usomaji wake na kuweza kubaini namna Majaliwa alivyohuzunika mara baada ya marimba yake kuibiwa. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa matumizi ya takriri katika kazi ya fasihi kwa lengo la kutolea msisitizo jambo au kitu ambacho mtunzi anataka hadhira yake

ikimanikie na kukizingatia zaidi. Kwa muktadha wa dondoo hapo juu wasomaji tunatakiwa kuzingatia kwamba Majaliwa alihuzunika mno mara baada ya marimba yake kuibiwa na mpinzani wake anayejulikana kwa jina la Kongoti.

Kama ilivyosemwa hapo awali kuwa matumizi ya takriri yamejitokeza katika sehemu nyingi za riwaya ya Marimba ya Majaliwa ni kweli. Katika dondoo lifuatalo kuna matumizi ya takriri:

> *…Majaliwa amfuate. Majaliwa, akiwa bado kapumbaa alisimama na kumwangalia bibi yake akitembea hadi alipofika maji ya magoti na kumgeukia Majaliwa na kuanza kuimba:*
> *Mjukuu wangu, mpendwa Majaliwa,*
> *Wahenga twasema, atakaye cha uvunguni Sharti ainame.*
> *Panda mgongoni, tufunge safari,*
> *Na tufunge safari, tufunge safari (*uk. 06).

Katika dondoo hili kuna marudio ya sentensi "tufunge safari," iliyorudiwa mara tatu. Hii inatoa msisitizo kwamba ni lazima marimba ya Majaliwa ipatikane kwa njia yoyote ile inayowezekana. Kupatikana kwa marimba hiyo ndiko kutakakomwezesha Majaliwa kushinda katika mashindano ya kitaifa ya upigaji wa marimba yatakayofanyika Dodoma kama inavyoelezwa katika riwaya teule. Marudiorudio haya yamejengwa kwa kutumia msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki kwa maana kwamba ndani ya safari husika kuna mambo ya msingi ya kufanya nayo si mengine bali ni kuhakikisha kuwa marimba ya Majaliwa inapatikana (Barthes, 1994). Hapa kunajitokeza dhamira ya dhati ya kutaka kufanikiwa kwa Majaliwa lakini hawezi kufanikiwa bila ya kufanya safari ya kuitafuta marimba yake iliyoibiwa. Hii pia, inamfanya msomaji mlengwa wa riwaya hii ambaye ni mtoto kutambua kuwa katika maisha ni lazima kufanya mambo bila ya kukata tamaa. Kukata tamaa husababisha kutofanikiwa katika maisha. Majaliwa alipanda katika mgongo wa bibi yake na mara moja safari ya kutafuta marimba ikaanza.

### 4.2.4 Matumizi ya Methali

Methali ni moja kati ya vipera vya semi ambacho pia hutumika kama mtindo wa lugha katika kazi za fasihi. Methali ni semi fupi ambazo huwa na pande mbili, yaani upande mmoja huwa ni kama swali na upande wa pili huwa ni jibu la swali hilo (Msokile, 1992). Mfano wa methali ni “haba na haba hujaza kibaba,” “asiyesika la mkuu huvunjika guu” na “asiye na mwana aeleke jiwe.” Methali hutumika katika kazi ya fasihi kama riwaya ili kutoa funzo fulani kwa hadhira wa kazi husika. Katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*, kuna matumizi ya methali kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> *“Majaliwa, usiogope. Ni mimi bibi yako nimekuja kukuchukua twende Unguja Kusini. Haya simama.”*
> *Ajabu, sauti kweli ilifanana na ya bibi yake. Majaliwa akashusha pumzi, akafarijika na kusimama. Bibi yake akageuka kuelekea baharini, akaanza kutembea juu ya maji …*
> *Mjukuu wangu, mpendwa Majaliwa,*
> *Wahenga twasema, atakaye cha uvunguni Sharti ainame.*
> *Panda mgongoni, tufunge safari,*
> *Na tufunge safari, tufunge safari* (uk. 06).

Maneno ambayo yameandikwa kwa kutumia wino wa kukolezwa ni methali ya Kiswahili. Methali hii inasisitiza juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa bila ya kuchoka. Pia, inasisitiza kuwa katika maisha kuna changamoto nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na si kuzikimbia au kuziogopa. Mtu anapotaka kuchukua kitu ambacho kiko katika uvungu wa kitanda au kitu kingine ni lazima mtu huyo ainame ndio aweze kukichukua au hata kukiona kitu hicho. Mtoto ambaye ndiye hadhira lengwa ya kitabu hiki anaposoma riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* na kukutana na methali hii, anapata kujifunza kuwa maisha yanahitaji uvumilivu wa hali ya juu ili kuyaishi vizuri. Mtu ambaye atakata tamaa baada ya kukumbana na

changamoto za maisha hawezi kuwa na mafanikio katika maisha yake. Methali hii imejengwa kwa kutumia msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki ambapo tukio la mtu kuinama kwa ajili ya kuchukuwa kitu katika uvungu linafananishwa kiishara na kuwa katika maisha kuna changamoto na hivyo hakuna njia ya mkato bali ni kupambana na changamoto hizo.

Methali ni kipera cha fasihi simulizi ambacho hupendwa kutumiwa na watoto katika michezo yao ikiwemo ile ya redioni. Hii ni kwa sababu methali husaidia kuwakuza watoto kisaikolojia na kifikra. Edwin Semzaba aliliona hili ndio maana katika riwaya yake ya *Marimba ya Majaliwa* iliyolengwa kwa watoto ina matumizi ya methali. Mfano mwingine wa matumizi ya methali ni huu ufuatao:

> *"Mjukuu wangu, mbona huna shukurani? Hebu jifunze kuwa na shukurani!" "Shukurani ya nini bibi?" Majaliwa aliuliza kwa mshangao. "Wewe subiri tu. Subira yavuta heri, "bibi alimjibu* (uk. 19).

Methali "subira yavuta heri," ndio iliyotumika katika dondoo lililopo hapo juu ambayo kimsingi imewekwa pale kwa lengo la kumfanya mtoto ambaye ndiye mlengwa mkuu wa riwaya hii kufahamu kwamba subira ni kitu muhimu katika maisha. Mtoto mdogo anapojifunza umuhimu wa kuwa na subira mara nyingi hufanikiwa katika maisha ya baadae ukubwani kwani hatofanya mambo kwa pupa na kumfanya kupata hasara badala ya faida katika kila jambo atakalolifanya. Hata hivyo si kila kitu kinapaswa kusubiriwa tu, kwani vipo baadhi ya vitu ambavyo vinahitaji kufanywa kwa uharaka. Majaliwa alimshangaa bibi yake alipomtaka kuwa na subira wakati yeye alitaka kuona mambo yanafanyika harakaharaka na anaipata marimba yake iliyoibwa na Kongoti. Kumshangaa huko bibi yake kulimsaidia kupata jibu

ambalo lilimuusia kuwa na subira. Watoto wote katika jamii wakipata mafunzo kama haya maisha yao ya baadae yatakuwa mazuri kwani hawatakuwa na tamaa za kupitiliza.

### 4.2.5 Matumizi ya Kiswahili cha Kimaeneo

Kiswahili ni lugha pana ambayo inazungumzwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa namna tofautitofauti kulingana na maeneo husika. Hata katika nchi nyingi duniani ambapo Kiswahili kinatumika, huzungumzwa kwa namna tofautitofauti. Hii ni kwa sababu wapo watu ambao Kiswahili si lugha yao ya kwanza na hivyo, kuweza kutamka maneno ya Kiswahili kwa usanifu wake ni kitu ambacho hakiwezekani mpaka pale watakapokaa na Waswahili wenyewe na kujifunza wanavyozungumza. Kitu hiki huchukua muda mrefu na mara nyingi huwa si rahisi kwani wapo hata wasomi wa lugha ya Kiswahili ambao nao hawawezi kutamka vizuri maneno ya Kiswahili sanifu. Katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kuna matumizi ya lugha ya kimaeneo na hapa tumetoa mfano wa jamii ya Wamaasai kama ifuatavyo:

> *Walitembea huku wakigeuka kuangalia nyuma kila wakati. Punde morani sita wa Kimasai walitokea na walipomuona Majaliwa pale juu ya mti hawakushangaa sana. "Rafiki ogopa simba?" Mmoja alisema kwa dhihaka. Mjaliwa hakujibu. ...*
> *"Iko simba ngapi?" "Wawili."*
> *"Wawili tu? Mbona iko peke yako mtoto?" "Niko peke yangu."*
> *"We umekuwa Morani hata hapana ogopa! Msitu ni mali ya Morani na simba peke yao. Sikia?"*
> *..."Chukua toto hii Singida," Mmaasai mmoja alimwambia dereva.*
> *"Hapana," Majaliwa alisema haraka. "Mimi nakwenda Babati* (uk. 99)."

Dondoo hili lina matumizi ya lugha ya Kiswahili katika eneo la jamii ya Wamaasai ambapo tunaona bayana kuwa Kiswahili chao ni tofauti na Kiswahili sanifu.

Ushahidi wa matumizi ya lugha ya aina hii ni pale anaposema, “rafiki iko ogopa simba,” “iko simba ngapi,” “mbona iko peke yako mtoto,” “hapana ogopa,” na “chukua toto hii Singida.” Maneno haya ni uthibitisho wa kuwepo mtindo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kulingana na maeneo. Msomaji anapokutana na maneno haya anaipata vizuri ladha ya lafudhi ya Kimaasai na kisha kuulewa ujumbe ambao umelengwa na mwandishi aupate. Matumizi ya mtindo wa lugha ya aina hii katika riwaya unaifanya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kuwa ni riwaya hai na inaendana na mazingira ya halisi ya kile inachokieleza.

Kimsingi, katika sehemu hii tumewasilisha, kuchambua na kujadili data ambazo zinahusiana na lengo mahususi la kwanza la utafiti wetu. Lengo hilo lilitaka kubainisha matumizi ya vipengele vya mtindo vya lugha na kwa kiasi kikubwa tumefanikisha. *Marimba ya Majaliwa* ni riwaya ya watoto ambayo kwa kweli ina sifa zote muhimu za kimtindo ambazo zinaifanya kuwa riwaya ya watoto. Riwaya hii ikisomwa na watoto wanaweza kujifunza mambo mazuri ambayo yanawasilishwa kupitia matumizi ya mtindo katika matumizi ya lugha tulioubainisha. Sehemu inayofuata inahusu matumizi ya vipengele vingine vya kimtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.

## 4.3 Vipengele Vingine vya Kimtindo katika Marimba ya Majaliwa

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilihusu kubainisha vipengele vingine vya kimtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Tuliamua kuwa na lengo hili kwa sababu kuna matumizi makubwa ya mtindo katika riwaya teule na tukaona kuwa njia

muafaka ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na lengo maalumu linaloshughulikia kipengele hiki.

### 4.3.1 Matumizi ya Nyimbo

Katika riwaya teule kuna matumizi makubwa ya kipengele cha nyimbo ambazo zinajitokeza karibu katika kila sura. Nyimbo ni moja kati ya kipengele cha kimtindo pale kinapotumika katika riwaya, hadithi au tamthiliya. Katika ukurasa wa kwanza tu wa riwaya teule kuna matumizi ya nyimbo. Mwandishi anasema:

> *Hapakuwa na shaka yoyote kuwa Majaliwa atakuwa ameshinda shindano lile la mkoa, kwani umati uliofurika kwenye uwanja wa michezo wa Mafia ulimshangilia kwa nguvu mara alipomaliza kupiga wimbo wake kwa kutumia marimba:*
> *Mie Majaliwa naimba*
> *Nimejaliwa kuimba*
> *Kwa haya yangu marimba*
> *Mapigo yenda sambamba*
> *Naomba nipeni mji*
> *Asilani sitaki kijiji*
> *Daima nalitaka jiji*
> *Kwani mie sishikiki*
> *Majaliwa ninaimba*
> *Ninaimba kwa kutamba*
> *Nawapa kwenye dimba*
> *Tumbuizo la marimba (*uk. 01).

Wimbo huu umetumiwa kama nyenzo ya kimtindo ambapo mwandishi ametudhihirishia kuwa Majaliwa alikuwa ni bingwa wa kuimba. Kutokea kwa wimbo huu mwanzoni kabisa mwa riwaya kunaweza kuelezwa kama korasi ikiwa na maana kuwa kila kitu ambacho kimetokea ndani ya riwaya kinahusiana na wimbo huu. Jambo hili si uongo bali ni ukweli kwani riwaya nzima ya *Marimba ya Majaliwa* inazungumzia kisa cha Majaliwa kutafuta marimba yake ambayo imeibwa na Kongoti ambaye ni mpinzani wake. Majaliwa aliamua kuimba wimbo huu kama

njia ya kuwaogopesha wapinzani wake ambapo tunaona kweli Kongoti aliogopa na ndipo alipoamua kuiba marimba ya Majaliwa. Baada ya kuiba marimba hayo ndipo msako ukaanza ambapo Majaliwa alisafiri sehemu mbalimbali kulikokuwa na mashindano ya kuimba na kupiga marimba, ambako Kongoti alishiriki. Matumizi ya wimbo huo yametengeneza korasi nzuri ndani ya riwaya kama asemavyo Mutembei (2012) kuwa nyimbo hutumiwa kama korasi ya kuelezea mambo ambayo yatatokea baadae ndani ya kazi ya fasihi. Ili msomaji au msikilizaji aweze kuifahamu korasi na dhima yake, ni lazima asome kwa makini kazi husika.

Matumizi ya nyimbo yanajitokeza katika sehemu mbalimbali ndani ya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ambapo tunaona katika ukurasa wa 3 kuna wimbo na ukurasa wa 4 pia kuna wimbo. Hata hivyo katika sehemu hii tumedondoa wimbo ambao upo ukurasa wa 8 kama ifuatavyo:

> *Majaliwa alimkumbatia bibi yake kama mkwezi wa mnazi, akashuhudia uhodari wa bibi wa kukata maji. Wimbo waliozoea kuimba shuleni ukamjia, naye akauimba kimoyomoyo:*
> *Nahodha ni Abdala, ni mtu mwema sana*
> *Hakuna kama yeye, kwa uadili na utii*
> *Kwa uadili na utii.*
> *Siku moja Abdala, alilewa pombe sana*
> *Katumbukia baharini, kichwa kikaliwa na papa*
> *Kikaliwa na papa* (uk. 08).

Wimbo huu umetumika kama sehemu ya mtindo lakini unaelezea umuhimu wa mtu kuzingatia maadili mema katika jamii. Mhusika Abdala anayetajwa katika wimbo huu, inabainishwa kuwa aliwahi kuwa mtu mtiifu na muadilifu kwa kiwango kikubwa lakini siku moja aliasi na kujiingiza katika ulevi. Baada ya kujiingiza katika ulevi aliishia kupata maangamizi ya kuliwa na papa baharini. Mtoto mdogo kama

Majaliwa anapouimba wimbo huu anajifunza kuwa ulevi si kitu kizuri kwani saa yoyote huweza kumfanya mtu akadhurika. Mtunzi ameujenga wimbo huu kwa kutumia msimbo wa kimatukio ambapo tukio la ulevi limetumika ili kufikisha ujumbe kwa hadhira kuwa ulevi haufai. Watoto wote watakaosoma riwaya hii watajifunza kwamba kujiingiza katika ulevi ni kinyume na maadili na hivyo si jambo zuri la kuigwa.

### 4.3.2 Matumizi ya Hadithi Ndani ya Hadithi

Hadithi ndani ya hadithi ni miongoni mwa mtindo mkongwe ambao umekuwa ukitumika katika fasihi simulizi tangu hapo kale. Ni jambo la kawaida katika fasihi simulizi kuona hadithi kuzua hadithi nyingine ndani yake na kuanza kuisimulia hadithi hiyo mpya. Hadithi hiyo mpya huweza pia kuibua hadithi nyingine na hali huendelea hivyo. Watunzi wa kazi za fasihi andishi nao pia hutumia mtindo huu katika kazi zao. Dondoo lifuatalo linathibitisha matumizi ya mtindo wa hadithi ndani ya hadithi kama ifuatavyo:

> *… "Bibi, kwa nini babu anakuchukia?" "Nitakueleza mjukuu wangu," bibi alijibu. Alikaa kimya kwa muda huku akimwangalia Majaliwa, kisha alianza kuongea.*
> *"Paukwa!*
> *Majaliwa akajibu, "Pakawa."*
> *Hapo kale babu yako alikuwa mume wangu. Alinitesa sana. Wakati huo tuliishi duniani. Babu alikuwa na mke mwingine, hivyo akawa hanijali mimi. Siku moja yeye na mkewe huyo wa pili walikula njama. Nilipokwenda kisimani wakati wa kuchota maji wakati wa usiku, walinitumbukiza kisimani nikafariki. Nikaenda kuzimu ambako nilikuwa na bidii hata wengi wakanipenda. Naye babu yako alipokufa akaja kuzimu, lakini kutokana na matendo yake mabaya alipokuwa duniani, akawekwa daraja la saba kwenye dhiki nyingi. …* (uk. 23-24).

Hapa katika dondoo hili kunasimuliwa hadithi kuhusu maisha ya ndoa na baadae kuzimu ya bibi na babu yake Majaliwa. Tukiitazama hadithi hii tunaiona ikiwa imeanza kwa kufuata kanuni za fasihi simulizi ambapo hadithi huanza na maneno "paukwa," kutoka kwa msimulizi na hadhira huitikia "pakawa." Huu ni ushahidi tosha kwamba hapa kuna matumizi ya mtindo wa hadithi ndani ya hadithi. Pia kisa ambacho kinasimuliwa hakimuhusu Majaliwa bali kinamhusu bibi na babu yake. Kimsingi, hadithi hii imetumika kwa lengo la kumjenga mtoto kuwa mtenda mema katika maisha yake yote ya duniani ili aweze kuishi vizuri maisha ya baada ya kufa huko kuzimu. Haya ni mafunzo ambayo hata katika vitabu vya dini yanaelezwa bayana na kwamba kama kila mtu katika jamii anaaswa kuishi kwa kutenda matendo mema.

Matumizi ya hadithi hii ndani hadithi yamesaidia sana kuleta ushikamani katika visa na matukio katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Kupitia hadithi hii tumeweza kufahamu ni kwa nini bibi alikuwa akimchukia sana babu na pia ni kwa nini babu alimwezesha Kongoti kuiba marimba ya Majaliwa. Hadithi hiyo ya "paukwa na pakawa" ni moja kati ya vitu ambavyo vinapendwa na watoto. Kuwepo kwake katika riwaya teule kunawafanya watoto ambao ndio walengwa wakubwa wa riwaya hii kuisoma bila ya kuchoka. Kadri wanavyoendelea kuisoma ndivyo wanavyoelewa dhamira zilizolengwa kwao kama watoto.

### 4.3.3 Mwingiliano Matini katika Riwaya ya Marimba ya Majaliwa

Mwingiliano matini ni mtindo katika utunzi wa kazi za fasihi ambapo matini moja huingia ndani ya matini nyingine ya fasihi. Hapa tuna maana kuwa inawezekana kazi

iliyopo mbele ya msomaji ni riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* lakini ndani yake mna habari kutoka katika riwaya nyingine ya mtunzi huyo huyo au mwingine. Mtindo huu husaidia kuifanya kazi ya fasihi inayosomwa kwa wakati huo kuwa hai zaidi na hatimaye kuwavutia wasomaji wake. Mwandishi Edwin Semzaba ni mmoja kati ya watunzi ambao wamekuwa wakitumia mtindo wa aina hii na ufuatao ni mfano dhahiri:

> *Majaliwa aliimba huku akifanya kazi kwa nguvu… walishangazwa na umahiri wake wa kuimba. Alisikia mmoja wao akiuliza, "kwa nini asingeingia kwenye mashindano ya kuimba huko mjini?" … Hawa ndio Siti Binti Saad, hawa. Waimba kama chiriku. Siti alianza kuimba wakati akiuza vitumbua, mpaka akaja kuwa mwimbaji mashuhuri, Unguja haijapata kuona!"*
> *Msemaji alianza kutamba:*
> *"Siti binti Saad*
> *Ulikuwa mtu lini?*
> *Ulitoka shamba*
> *Na kaniki mbili chini*
> *Kama si sauti*
> *Ungekula nini* (uk. 11)?"

Katika dondoo hili tunaona Siti Binti Saad akitajwa kuwa alikuwa ni mwimbaji maarufu wa nyimbo za taarab huko Zanzibar na baadae Afrika na duniani kote. Huyu ni mhusika katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* iliyoandikwa na Shaaban Robert. Pia, kumedondolewa sehemu ya wimbo kutoka katika *Wasifu wa Siti Binti Saad* na kutiwa katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kama inavyoonekana hapo juu. Mwingiliano huu wa tanzu umefanywa kwa makusudi ili kuhakikisha kuwa hadhira inaipata vizuri dhana ya kuwa Majaliwa alikuwa mwimbaji mwenye kipaji kikubwa aliyemkaribia Siti Bainti Saad. Ikitokea kwa bahati ikawa mtu anayesoma riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* amewahi kusoma pia riwaya ya *Wasifu Binti Saad* inakuwa rahisi kwake kuelewa kile ambacho mwandishi anataka msomaji akielewe.

### 4.3.4 Mtindo wa Tanzu Ndani ya Tanzu Ndani ya Tanzu

Riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* imeundwa kwa mtindo wa kipekee ambapo tumeona kuwa kuna matumizi ya mtindo wa tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu. Ukiyatazama maneno haya kwa haraka unaweza kusema mbona yanarudiwarudiwa bila sababu. Urudiaji wa maneno hayo haujakosewa uko sawa kwani kinachosemwa hapa ni tanzu tatu zimeingiliana kwa wakati mmoja. Tunaposoma riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* tunabaini kuwa kuna matumizi ya nyimbo ambapo ndani yake mna methali na vyote hivi vipo ndani ya utanzu wa riwaya. Hapa ndipo dhana ya tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu inapotokea. Tuone mfano ufuatao:

> *Ajabu, sauti kweli ilifanana na ya bibi yake. Majaliwa akashusha pumzi, akafarijika na kusimama. Bibi naye akageuka kuelekea baharini, akaanza kutembea juu ya maji huku akimtaka Mjaliwa amfuate. Majaliwa akiwa bado kapumbaa, alisimama na kumwangalia bibi yake akitembea hadi alipofika maji ya magoti na kumgeukia Majaliwa na kuanza kuimba:*
> *Mjukuu wangu, mpendwa Majaliwa*
> *Wahenga twasema, atakaye cha uvunguni sharti ainame.*
> *Panda mgongoni, tufunge safari*
> *Na tufunge safari, tufunge safari.*
> *Bibi aliimba kwa sauti ya kuvutia kiasi kwamba Majaliwa alijikuta akipanda mgongoni kwa bibi yake kama vile ni tumbili kwa mamaye* (uk. 06-07).

Dondoo hili ndani yake kuna wimbo ambao upo katika riwaya ulioimbwa na bibi yake Majaliwa ili kumbembeleza Majaliwa apande mgongoni. Katika wimbo pia kuna matumizi ya methali isemayo, “atakaye cha uvunguni sharti ainame,” na hivyo kuwa utanzu ndani ya utanzu. Mtindo huu unasaidia katika kuifanya hadhira kuelewa vizuri ujumbe unaowasilishwa kwao na mwandishi. Sambamba na hilo, matumizi ya mtindo wa aina hii yanasaidia watoto ambao ndio walengwa wa riwaya hii kuelewa dhamira kwa urahisi. Imekuwa ni kawaida kwa watoto kupenda sana nyimbo na

hivyo methali zinapowekwa ndani ya nyimbo ni njia nzuri ya kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Ujumbe unaopatikana katika dondoo hapo juu ni kuwataka watoto pamoja na watu wengine katika kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili wawe na maisha mazuri. Maisha mazuri hayapatikani kwa njia za ujanjaujanja na wizi bali ni kwa kujituma na kufanya kazi kwa bidii. Hivyo, mtindo wa tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu umejidhihirisha pale ambapo wimbo ni utanzu uliopo ndani ya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* na ndani ya wimbo kuna utanzu mwingine wa methali.

### 4.3.5 Mtindo wa Uhalisia Mazingaombwe

Uhalisia mazingaombwe ni mtindo unaotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kwa kuelezea dhamira katika kazi kwa kutumia visa na matukio ambayo hayaaminiki kutokea katika ulimwengu wa kawaida (Senkoro, 2006). Mtindo huu ulianza kutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi tangu zamani na hata riwaya za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Kufikirika* nazo pia zimeandikwa kwa kutumia mandhari ambayo ni ya kiuhalisia mazingaombwe (Mbatiah, 1998). Riwaya hizi zinazungumzia nchi ambayo ipo angani lakini yale yanayosemwa yanatokea katika ulimwengu wa kawaida. Watunzi wa siku za hivi karibuni kama Euphrase Kezilahabi amekuja na mtindo wa kiuhalisia mazingaombwe ambao ni wa kutatiza zaidi ikilinganishwa na mtindo wa Shaaban Robert. Katika riwaya zake za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) kuna matumizi ya mandhari ambayo ni tata na haielezeki kabisa.

Pia, kuna matumizi ya wahusika wasiosemeka, kuna visa na matukio ambayo hata kwa ndoto tu hayatazamiwi kutokea hapa duniani; mtoto anaongea akiwa bado tumboni kwa mama yake, mhusika ana mguu mrefu ambao hauna mwisho, kusikia

vicheko vya watu bila ya kuwaona watu hao na kuchapwa viboko bila ya kumuona mchapaji wa viboko hivyo (Wamitila, 2008).

Mwandishi Edwin Semzaba naye pia katika riwaya yake ya *Marimba ya Majaliwa* ametumia mtindo wa kiuhalisia mazingaombwe katika kuelezea visa na matukio mbalimbali ndani ya riwaya yake ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyolengwa. Dondoo lifuatalo ni mfano mzuri unaothibitisha mawazo haya:

> *Majaliwa hakujibu onyo la bingwa wa taifa. Alirudi nyumbani kwao huku akiwa amekumbatia marimba yake. Giza lilianza kuingia. Upepo uliotokea baharini ulimpiga usoni na kumfurahisha sana. Mara alishtukia anapigwa ngwara na kuanguka. Marimba aliyokuwa ameyakumbatia yakamtoka mikononi. Kutahamaki alisikia vishindo vya miguu ya watu waliokimbilia vichakani. Majaliwa aliinuka na kuangalia pande zote. Lahaula! Hakuona marimba yake, yalikuwa yamechukuliwa! Alisikitika sana (uk. 02).*

Dondoo hili linabainisha kuwa Majaliwa alinyang'anywa marimba yake na watu ambao hakuwahi kuwaona lakini walimpiga ngwara na kuondoka zao. Katika maisha halisi si jambo la kawaida mtu kupigwa ngara akaanguka chini na kisha akanyang'anywa kila kitu bila ya kumuona huyo ambaye amefanya kitendo hicho, labda iwe macho yake yalifungwa. Hata hivyo, hakuna mahali ambapo tunaambiwa kuwa macho ya mhusika Majaliwa yalifungwa au kuzibwa ili asione kile ambacho kinaendelea. Huu ni uhalisia mazingaombwe ambapo mtunzi ametumia msimbo wa kimaelezo kuelezea suala hili. Tukio la kupigwa ngwara na kunyang'anywa marimba yake Majaliwa ni tukio la kiishara ambalo linamaanisha kuwa katika maisha kuna changamoto nyingi na hivyo ni lazima kujitahidi ili kupambana na changamoto hizo. Matumizi mengine ya mtindo wa kiuhalisia mazingaombwe yanajitokeza katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kama ilivyo katika dondoo lifuatalo:

> *Hapo hapo, safari ilianza, bibi akaanza kwenda juu ya maji kwa mwendo wa kasi. Majaliwa hakuamini, lakini baada ya muda mfupi alianza kufurahia safari (uk. 07).*

Dondoo hili linaonyesha kuwa bibi yake Majaliwa alikuwa na uwezo wa kusafiri juu ya maji kama vile meli kitu ambacho kwa uhalisia si sahihi. Katika maisha ya kawaida hakuna mtu ambaye anauwezo wa kusafiri juu ya maji bila ya kutumia chombo chochote cha usafiri wa majini lakini tunaelezwa kuwa bibi yake Majaliwa aliweza. Tukio hili nalo limejengwa kwa kutumia msimbo wa kiishara ikiwa na maana kwamba kitu chochote katika maisha kinawezekana ila jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba jitihada inafanyika. Hata vitu ambavyo katika mazingira halisi vinaonekana kuwa haviwezi kufanyika lakini jitihada huweza kusaidia kupatikana kwa maarifa ya kushughulikia tatizo au changamoto husika. Haitakiwi kukata tamaa hata mara moja katika maisha. Mtoto ambaye ni mlengwa wa riwaya hii ya Marimba *ya Majaliwa* anaposoma riwaya hii anapata uelewa kuwa kila kitu katika maisha kinawezekana pale tu mtu huyo atakapoamua kukifanya kitu hicho.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa namna ambayo imesaidia kujibu maswali ya utafiti wetu kupitia kukamilika kwa malengo mahususi ya utafiti. Katika lengo mahususi la kwanza la utafiti huu tumefanikiwa kubainisha vipengele vitano vya mtindo wa lugha katika riwaya teule. Vipengele hivyo ni tashibiha, chuku, takriri, methali na Kiswahili cha kimaeneo. Katika lengo mahususi la pili tumebainisha vipengele vingine vya kimtindo ambavyo ni matumizi ya nyimbo, hadithi ndani ya hadithi, mwingiliano matini, tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu na matumizi ya uhalisia mazingaombwe.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho katika tasinifu yetu ambayo imewasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari

Uwasilishaji katika sura hii umefanywa kwa kuzingatia madhumuni mahususi ya utafiti huu ambayo yalikuwa mawili. Malengo hayo yalikuwa ni kubainisha vipengele vya mtindo vya matumizi ya lugha katika riwaya teule na kubainisha vipengele vingine vya matumizi ya mtindo katika riwaya teule.

### 5.2.1 Vipengele vya Kimtindo vya Matumizi ya Lugha

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha vipengele vya kimtindo katika riwaya teule. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa vipengele vya kimtindo vya matumizi ya lugha vinajitokeza kwa kiasi kikubwa katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*. Vipengele hivyo ni pamoja matumizi ya tashibiha, chuku, takriri, methali na Kiswahili cha kimaeneo. Vipengele hivi kwa umoja wake vimesaidia kujenga dhamira zinazowahusu watoto kwa kuwa ndio walengwa wakubwa wa kazi hii nzuri ya Edwin Semzaba. Mathalani, katika upande wa tashibiha tumebaini kuwa mwandishi ametumia tashibiha ambazo zinahusu ndege kama vile chiriku na jogoo. Jogoo ni kuku dume ambaye hufugwa nyumbani na

watoto huwaona kila siku wanapokuwa katika michezo yao. Hii inaifanya riwaya husika kuwa ni riwaya iliyo karibu na hadhira yake.

Pia, kuna matumizi ya chuku ambayo yamejitokeza katika riwaya teule ambapo tunaelezwa kuwa bibi yake Majaliwa alikuwa ni mtu awezaye kutoa ushuzi unaosababisha wanadamu kuzimia kwa muda wa siku tatu. Hii kwa hakika si kitu ambacho kinaweza kuaminiwa katika ulimwengu wa kawaida lakini kwa watoto huweza kuaminika. Lengo la kutumiwa kwa chuku hii ni kuwafanya watoto watakaosoma riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kuamini kuwa bibi ni mtu mwenye uwezo wa kufanya kila kitu na hata siku moja huwa hashindwi. Mtoto akiamini hivi anakuwa na heshima kwa bibi na watu wengine wenye umri kama wa bibi.

### 5.2.2 Vipengele vingine vya Kimtindo katika Riwaya Teule

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilihusu kubainisha vipengele vingine ambavyo si vya matumizi ya lugha katika riwaya teule. Vipengele vilivyobainishwa ni pamoja matumizi ya nyimbo, hadithi ndani ya hadithi, mwingiliano matini, tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu na uhalisia mazingaombwe. Vipengele hivi vimesaidia sana katika kuwasilishwa dhamira kwa hadhira ya riwaya teule ambayo ni watoto. Nyimbo zimetumika kwa kiasi kikubwa sana katika riwaya hii kwa sababu nyimbo ni kitu kinachopendwa sana na watoto. Kutumika kwa nyimbo kunaifanya riwaya kueleweka kwa urahisi zaidi kwa kuwa katika nyimbo kunafumbatwa dhamira mbalimbali. Pia, tumeona matumizi ya tanzu ndani ya tanzu ndani ya tanzu ambapo tanzu tatu zimeingiliana na kutumika kwa pamoja. Hii ni njia nzuri ya kuiteka

hadhira ya riwaya hii kwani msomaji anakuwa hachoki kuisoma na akianza kusoma hawezi kuiweka chini.

## 5.2 Hitimisho

Kwa jumla utafiti wetu umekamilika baada ya kukamilika kwa malengo mahususi mawili ya utafiti huu. Riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* kwa kweli inastahili kuitwa kuwa ni riwaya ya watoto. Hii ni kwa sababu imetungwa kwa kutumia mtindo ambao unaendana na mahitaji ya watoto. Matumizi ya mtindo wa kiuhalisia mazingaombwe unapendwa na watoto na hutoa mafunzo mazuri kwao. Riwaya hii imejaa visa na matukio ambayo ni ya kiuhalisia ajabu lakini ndani yake kuna mafundisho makubwa. Miongoni mwa matukio hayo ya kiuhalisia mazingaombwe ni pamoja na bibi kutoa ushuzi ambao unaweza kuwafanya watu wasikiao harufu hiyo kuzimia, bibi kusafiri juu ya maji ya bahari bila chombo cha usafiri na Majaliwa kupigwa ngwara bila ya kumuona mtu aliyempiga. Watoto wanaposoma riwaya hii na kukutana na matukio haya hawaishii tu kucheka lakini pia hujifunza mambo mbalimbali kuhusu maisha.

## 5.3 Mapendekezo

Tunapendekeza kuwa utafiti kama huu wetu unaweza kufanywa katika riwaya nyingine zinazowahusu watoto ili kuona nako kuna matumizi ya mtindo wa aina gani. Pia, watafiti wajao wanaweza kufanya utafiti linganishi kwa kulinganisha riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* na riwaya nyingine za watoto katika kipengele cha mtindo na vipengele vingine.

**MAREJELEO**


Babie, E. (1999), *The Basics of Social Research*, Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Barthes, R. (1994), *The Semiotic Challenge*, Berkely: University of Califonia Press.

Chandler, D. (1992), *Semiotics: The Basics*, London: Routledge Press.

Cobley, P. (2001), *The Routledge Companion to Semiotics and Linguistics*, London: Routledge.

Cohen, L. *et. al*. (2000), *Research Methods in Education* (5th end) London: Routledge.

Creswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*, Los Angeles: SAGE Publications.

Ebrahim, H. (1972), *Mashetani*, Nairobi: EALB.

Eco, U. (1976), *A Theory of Semiotics.* Bloomington: Indiana University Press.

Hawthorn, J. (1985), *Studying the Novel: An Introduction*, New Delhi: Universal Book Stall.

Kezilahabi, E. (1990), *Nagona*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991), *Mzingile*, Dar ear es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khamis, S. A. M. (2007), "Utandawazi au Utandawizi?: Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai," katika *Kiswahili*, Juzuu namba 70, Dar es Salaam: TUKI, Kur.47-66.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A (2006), *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Pauliness Publications.

Kothari, C. R. (2008), *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques*, New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Madumullah, J. S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi,* Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Mark, G. (1995), *Postmodern semiotics: Material culture and the forms of postmodern life.* Oxford: Basil Blackwell.

Mbatiah, M. (1998), "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*," *Mulika* namba 24, TUKI, Kur. 1-11.

Mlacha, S. A. K. (1989), "The Use of Methaphor in Kezilahabi's Novel: *Rosa Mistika*," katika *Kiswahili*, Juzuu namba 56, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 25-35.

Mlacha, S. A. K. (1991), "Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels," in *Kiswahili* Vol. 58, Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mlacha, S. A. K. (1996), "Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya *Bwana Myombekere* na *Bibi Bugonoka*," katika, *Mulika* namba 23, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 24-35.

Mohamed, M. (2006), Mtindo katika Riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*," katika *Kioo cha Lugha,* Juzuu namba 4, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 1-12.

Msokile, M. (1992), *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Education Publishers and Distributor, Ltd.

Msokile, M. (1993), *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya,* Dar es Salaam: DUP.

Mulokozi, M. M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili,* Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2008), "Dibaji katika *Marimba ya Majaliwa*," Dar es Salaam: E&D Vision Publishing.

Mwamzandi, I. (2013), “Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi,” katika *Swahili Forum* 20:48-66.

Mwijande, G. (2012), “Dhima ya Ucheshi katika Kuibua Visa na Maudhui: Uchambuzi wa Riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*,” Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999), *Ufudishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: JKF.

Onchangu, R. N. (2013), “Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi,” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Robert, S. (1951), *Kusadikika*, London: Nelson.

Robert, S. (1967), *Kufikirika*, Nairobi: OUP.

Robson, C. (2007), *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Semzaba, E. (2008), *Marimba ya Majaliwa*, Dar es Salaam: E&D Vision Publishing.

Senkoro, F. E. M. K. (2006), “Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi”, katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Walibora, K. W. (2010), “Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Duniya Yao* na *The Tin Drum*,” katika, *Swahili Forum* 17:143-157.

Wamitila, K. W. (2008), *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Wamitila, K. W. (2013), “Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili,” katika *Mulika* namba, 32, TATAKI: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Wanyonyi, M. C. (2011), “Uhakiki wa Riwaya ya *Nyunso za Mwanamke* na Said Ahmed Mohamed: Mtazamo wa Saikolojia Changanuzi,” Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Yin, R. K. (2001), *Case Study Research: Design and Methods*, (2$^{nd}$ eds.) Thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P. V. (1984), *Scientific Social Surves and Research*, Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.